



USAID
FROM THE AMERICAN PEOPLE



Kusoma Kiswahili

Kitabu Cha Mwanafunzi Cha 2



KUSOMA KISWAHILI: KITABU CHA MWANAFUNZI CHA 2



PHOTO: Christopher Steel

Kusoma Kiswahili Cha Mwanafunzi

Yaliyomo

Shukrani	ii	Wiki ya 15	71
Wiki ya 1	1	Wiki ya 16	76
Wiki ya 2	6	Wiki ya 17	81
Wiki ya 3	11	Wiki ya 18	86
Wiki ya 4	16	Wiki ya 19	91
Wiki ya 5	21	Wiki ya 20	96
Wiki ya 6	26		
Wiki ya 7	31	Wiki ya 21	101
Wiki ya 8	36	Wiki ya 22	106
Wiki ya 9	41	Wiki ya 23	111
Wiki ya 10	46	Wiki ya 24	116
		Wiki ya 25	121
		Wiki ya 26	126
Wiki ya 11	51	Wiki ya 27	131
Wiki ya 12	56	Wiki ya 28	136
Wiki ya 13	61	Wiki ya 29	141
Wiki ya 14	66	Wiki ya 30	146

Shukrani

Kitabu hiki cha wanafunzi kimefanikishwa kutokana na ufadhili wa DFID na USAID/Kenya. Katibu wa Kudumu wa Wizara ya Elimu Profesa George Godia alihusika sana katika kuelekeza juhudi za kitaaluma za Wizara ya Elimu, Baraza la Mitihani nchini Kenya (KNEC), Taasisi ya Wasimamizi wa Elimu ya Kenya (KEMI), Taasisi ya Elimu Maalum ya Kenya (KISE), na Tume ya Kuwaajiri Walimu (TSC). Kwa pamoja, DFID na USAID wanawasilisha kitabu hiki kwa Wizara ya Elimu kwa minajili ya utafiti katika shule zilizo chini mradi wa kuboresha ujuzi wa hisabati na usomaji nchini (PRIMR). **Kitabu hiki ni cha utafiti na matumizi yake nje ya shule zilizo kwenye mradi wa PRIMR hayaruhusiwi.**






Shukrani maalum zawaendea kikundi cha wataalamu kilichoandika kitabu hiki kutokana na mwongozo wa mawanda na mfuatano ulioundwa kwa ushirikiano na Wizara ya Elimu. Shukrani kwa Dkt. Sylvia Linan-Thompson kwa kuongoza uundaji wa mwongozo wa mawanda na mfuatano wa Kiswahili. Shukrani pia kwa kikundi saidizi cha kitaalamu kinachojumuisha Dkt. Agatha van Ginkel, Dkt. Hellen Inyega na Prof. Angelina Kioko. Hongera na shukrani pia kwa kikundi cha kitaalamu cha RTI PRIMR: Dkt. Benjamin Piper, Jody Roy, Titus Kazungu, Sarah Koko, Isaac Cherotich, Samuel Ogwang, Salome Ong'ele na Jessica Mejia kwa bidii yao katika kuandika kitabu hiki.

Shukrani maalumu ni kwa kikundi cha Uanzilishi na Utekelezi wa Mradi (PDIT) kinachojumuisha washiriki wa Wizara ya elimu na Wadau wengine. Kikundi hiki kiliongoza ruwaza ya mpango huu, uanzilishi wa mpangilio wa mawanda na mfuatano. Pia kiliandika mipangilio ya masomo na kinasimamia majaribio ya nyenzo hizo madarasani. Kikundi kingine kinajumuisha Washauri wa walimu (TAC Tutors), makocha, walimu katika shule za PRIMR kikundi cha kwanza. Mchango wao katika kuboresha nyenzo hizi unatambulika sana. Pia wanafunzi na washiriki wa jamii katika kaunti ya Nairobi, Kiambu, Nakuru na Kisumu walihusika kwa kiwango kikubwa. Ubora wa kazi hii unatokana na juhudi zao za dhati.




Shukrani pia kwa Masudi Ramadhan Abdi na Apollo Erik kwa uchoraji wa picha. Hatimaye ni bidii, uwezo na talanta ya wanafunzi wa nchi ya Kenya ambao watupa motisha kuendeleza na kufanikisha mradi huu.

Mei 2013

Siku ya 1

	M m	A a	U u
	j u ju	m u mu	m a ma
	m ju kuu m jo mba	mjukuu mjomba	ja maa jamaa sha nga zi shangazi
	wa li aga hu i andalia hu hudhuria		waliaga huiandalia huhudhuria
		mjukuu	jamaa

Siku ya 2





	K k	T t	L l
	Umoja mjomba shangazi	Wingi wajomba shangazi	Umoja mjukuu
			Wingi wajukuu
	mjukuu yuko	chini ya	meza
	binamu yuko	juu ya	kiti
	mjomba yuko	karibu na	kitanda
	shangazi yuko	mbele ya	kabati
	Babu yuko	kando ya	mti
	Umoja mjukuu jamaa	Wingi wajukuu jamaa	Umoja mjomba Shangazi
			Wingi _____ _____








Jamaa ya Bwana na Bi. Kasri


Bwana na Bi. Kasri wanaishi katika kijiji cha Kunguni na mjukuu wao Pendo. Pendo ni yatima. Wazazi wake waliaga dunia kutokana na ajali ya barabarani. Ingawa Pendo ni yatima, yeye anapendwa na kila mtu. Kila jioni yeye hucheza na binamu zake wawili. Pendo ana mjomba ambaye ni daktari katika hospitali ya Kunguni. Pia ana shangazi ambaye ni mwalimu katika shule ya malezi. Wakati wa likizo Bwana na Bi. Kasri huiandalia jamaa yao karamu. Karamu hiyo huhudhuriwa na kila mtu.

Siku ya 3

	N n	O o	W w
	n o no t o to	w a wa n a na	
	ma ra fi ki wa za zi bi na mu m ku bwa	marafiki wazazi binamu mkubwa	
	mjukuu	jamaa	

Siku ya 4

	E e	H h	I i
	e e	h e he	r e re
	ha di thi wa to to mo la sha i ri ho di	hadithi watoto mola shairi hodi	
	ku ni letea ni ta wa elezea tu sherehekee na wa heshimu	kuniletea nitawaelezea tusherehekee nawaheshimu	
	1. dithiha 4. ngazisha	2. lamo 5. mbamjo	3. mubina



Jamaa Yangu




Hodi hodi marafiki, shairi nawaletoa,
La baba na mama yangu, wazazi walonilea,
Majina ya jamaa yangu, yote nitawaeleza,
Ahsante Mola wangu, baraka kuniletea.

Kaka, dada umenipa, ndugu zangu wa pekee,
Na marafiki umenipa, tucheze tusherehekee,
Binamu ni watoto, wa mjomba na shangazi,
Ahsante Mola wangu, baraka kuniletea.





Shangazi, amu na mjomba, ndugu za baba na mama,
Si lazima kuwaomba, msaada wanatumana,
Baba mdogo, mkubwa, mungu ametuletea,
Ahsante Mola wangu, baraka kuniletea.

Wa mwisho na wa muhimu, waliozaa wazazi wangu,
Wananipenda nawaheshimu, babu na bibi yangu,
Hadithi zilizo tamu, michezo hucheza yangu,
Ahsante Mola wangu, baraka kuniletea.



Siku ya 5

★	<p>S s B b Y y</p>													
	<p>b a ba s i si y a ya</p>													
	<p>ba ba baba ma ma mama bi bi bibi ba bu babu m jo mba mjomba sha nga zi shangazi ja maa jamaa</p>													
	<table border="1"> <tr> <td>ba</td> <td>nga</td> <td>ja</td> <td rowspan="4">baba jamaa</td> </tr> <tr> <td>sha</td> <td>ma</td> <td>bu</td> </tr> <tr> <td>mba</td> <td>a</td> <td>Zi</td> </tr> <tr> <td>m</td> <td>bi</td> <td>Jo</td> </tr> </table>	ba	nga	ja	baba jamaa	sha	ma	bu	mba	a	Zi	m	bi	Jo
ba	nga	ja	baba jamaa											
sha	ma	bu												
mba	a	Zi												
m	bi	Jo												

Siku ya 1

★	Z z	D d	G g
	d a da g u gu	z i zi g a ga	z a za
	mu da ka zi	muda kazi	za ma ni zamani
	hu fanyia vi li vyo	tumiwa	hufanyia vilivyotumiwa
		muda	zamani

Siku ya 2






★	J j	R r	F f
		Umoja	Wingi
	Simu ya rununu hii ni	yangu	yetu
	Faksi hii ni	yangu	yetu
	Mashine ya chapa hii ni	yangu	yetu
	Printa hii ni	yangu	yetu
	Tarakilishi hii ni	yangu	yetu
	Simu ya waya hii ni	yangu	yetu
	Kupanga Silabi		
	1. musu	2. osifi	3. zika
	4. mazani	5. faavi	







Vifaa vya ofisi


Ofisi huwa na vifaa vya kufanya kazi mbalimbali. Vifaa hivi hufanya kazi kuwa rahisi. Watu hutumia tarakilishi kutuma barua pepe. Hapo awali watu walitumia simu za waya kuwasiliana. Sasa tuna simu za rununu ambazo zinaweza kutumika mahali popote. Njia hizi za kisasa za kutuma ujumbe zimerahisisha mawasiliano.

Siku ya 3

	Vv	sh	dh
	v o dh i	vo dhi	sh a sha
	vo cha		vocha
	u ta ka o ya me	thibitisha imarika	utakaothibitisha yameimarika
	thibitisha		bonyeza


Siku ya 4

	ny	ch	ng'
	ny e ch u ng' u	nye chu ng'u	ch o ch a cho cha
	bo nye za u li yo fi chu a u na cho hi ta ji		bonyeza uliyofichua unachohitaji
	1. musii 4. chafi	2. tishathibi 5. nyeboza	3. chavo



Jinsi ya kuweka muda wa maongezi kwenye simu ya rununu

Simu za rununu hutumika sana nchini mwetu. Unapotaka kutumia simu hiyo, hakikisha una fedha za kutosha kugharamia muda wa maongezi. Iwapo huna:

1. Nunua vocha ya kiwango cha muda wa maongezi unachohitaji.
2. Kwaruza sehemu iliyofichwa ili upate nambari ya siri.
3. Bonyeza alama ya *, nambari ya kampuni na alama ya * tena.
4. Bonyeza nambari ya siri uliyofichua ulipokwaruza kisha alama ya #
5. Sasa bonyeza alama ya  au OK.

Ngoja ujumbe utakaohitishwa kwamba simu yako iko tayari kutumika.





Siku ya 5

★	th gh ng													
☷	th a tha gh i ghi ng o ngo													
🏠	<table style="margin-left: auto; margin-right: auto;"> <tr> <td style="background-color: #333; color: white; padding: 5px;">da</td> <td style="background-color: #333; color: white; padding: 5px;">za</td> <td style="background-color: #333; color: white; padding: 5px;">cha</td> <td rowspan="4" style="padding-left: 20px; vertical-align: middle;"> muda zamani </td> </tr> <tr> <td style="background-color: #333; color: white; padding: 5px;">ma</td> <td style="background-color: #333; color: white; padding: 5px;">vo</td> <td style="background-color: #333; color: white; padding: 5px;">mu</td> </tr> <tr> <td style="background-color: #333; color: white; padding: 5px;">si</td> <td style="background-color: #333; color: white; padding: 5px;">a</td> <td style="background-color: #333; color: white; padding: 5px;">ni</td> </tr> <tr> <td style="background-color: #333; color: white; padding: 5px;">ba</td> <td style="background-color: #333; color: white; padding: 5px;">za</td> <td style="background-color: #333; color: white; padding: 5px;">ru</td> </tr> </table>	da	za	cha	muda zamani	ma	vo	mu	si	a	ni	ba	za	ru
da	za	cha	muda zamani											
ma	vo	mu												
si	a	ni												
ba	za	ru												





Technolojia



Siku ya 1

	m	
	m chi m pu nga m re fu m ge ni	mchi mpunga mrefu mgeni
	a ka m salimia ku m karibisha	akamsalimia kumkaribisha
	mchi	mpunga

Siku ya 2





	M			
	m chi m punga s ti ma m ge ni	mchi mpunga stima mgeni		
	Umoja mpunga mchi chakula chumba	Wingi mipunga michi vyakula vyumba		
	Umoja mpunga mchi mtoto	Wingi mipunga _____	Umoja chakula chumba	Wingi vyakula _____







Mgeni nyumbani

Jioni moja, Rehema alikuwa akitwanga mpunga kwenye kinu. Mchi aliokuwa akitumia kutwanzia ulikuwa mrefu. Naye alikuwa amesimama wima. Akamwona mgeni akiwasili langoni. Rehema akamsalimia na kumkaribisha kwenye chumba cha wageni. Aliwasha taa ya stima na kufungua televisheni ili mgeni astarehe. Rehema aliwasha moto haraka haraka na kupika wali na nyama ya kukaanga. Aliandaa chakula na kumkaribisha mgeni mezani. Mgeni alinawa na kupakua chakula baada ya sala. Rehema na mgeni wakala wali kwa nyama. Wakafurahi sana.

Siku ya 3

	n	
	nyimbo kwenda usingizi foronya angani	nyimbo kwenda usingizi foronya angani
	ki me tandikwa a li anza	kimetandikwa alianza
	Kujaza Pengo	
	1. kit_nda 4. r_dio	2. chak_la 5. g_doro
	3. for_nya	

Siku ya 4

	N	n
	blanketi foronya redio kusinzia	blanketi foronya redio kusinzia
	alianza alisinzia alipendeza	hakuanza hakusinzia hakupendeza
	alilala alisinzia aliimba alianza alikimbia	hakulala hakusinzia _____ _____ _____







Kapendo

Siku moja baada ya chakula cha jioni kapendo aliamua kusikiliza redio. Redio ilicheza nyimbo tamutamu. Bila ya kujua, Kapendo alianza kusinzia. Mama yake akaja na kusema, “Kapendo, amka. Kumbuka kunawa miguu yako kabla ya kulala. Sitaki uchafue blanketi lako la kujifunikia.” Kapendo alijibu, “Ndio mama.” Muda si muda, Kapendo alisinzia tena. Alianza kuota kuwa yuko kwenye kitanda chenye godoro zito na foronya nyororo. Kitanda hicho kilikuwa kinapaa angani. Alisikia sauti ya kupendeza ikimwita. Alipogutuka alimsikia mama akisema, “Mwanangu, amka. Nenda ukalale.”




Siku ya 5


★	ng' dh ny ng mb															
🗣️	dh a dha ny u nyu ng o ngo ng' o ng'o mb a mba															
📖	<table border="1"> <tr> <td>Kizee kiko</td> <td>chini ya</td> <td>meza</td> </tr> <tr> <td>Ng'ombe wako</td> <td>kando ya</td> <td>mwamba</td> </tr> <tr> <td>Mvulana yuko</td> <td>juu ya</td> <td>mti</td> </tr> <tr> <td>Baba yuko</td> <td>karibu na</td> <td>kisima</td> </tr> <tr> <td>Maji yako</td> <td>ndani ya</td> <td>chungu</td> </tr> </table>	Kizee kiko	chini ya	meza	Ng'ombe wako	kando ya	mwamba	Mvulana yuko	juu ya	mti	Baba yuko	karibu na	kisima	Maji yako	ndani ya	chungu
Kizee kiko	chini ya	meza														
Ng'ombe wako	kando ya	mwamba														
Mvulana yuko	juu ya	mti														
Baba yuko	karibu na	kisima														
Maji yako	ndani ya	chungu														
🏠	<table border="1"> <tr> <td>m</td> <td>ki</td> <td>do</td> <td rowspan="4">mchi godoro</td> </tr> <tr> <td>wi</td> <td>fo</td> <td>nda</td> </tr> <tr> <td>ro</td> <td>go</td> <td>chi</td> </tr> <tr> <td>ta</td> <td>mbo</td> <td>nya</td> </tr> </table>	m	ki	do	mchi godoro	wi	fo	nda	ro	go	chi	ta	mbo	nya		
m	ki	do	mchi godoro													
wi	fo	nda														
ro	go	chi														
ta	mbo	nya														

Siku ya 1

	dh	sh
	na dhi fu dha ha bu sa hi hi shia shu le ni	nadhifu dhahabu sahihishia shuleni
	ku fundishia	kufundishia
	sahihisha	mwalimu

Siku ya 2





	m	
	Umoja mwalimu huyu mtoto huyu mwanafunzi huyu	Wingi walimu hawa watoto hawa wanafunzi hawa
	Umoja mtoto huyu mwalimu huyu mtu huyu mvulana huyu	Wingi watoto hawa _____ _____ _____






Mwalimu wetu


Jina langu ni Kajuzi. Niko katika darasa la pili shuleni Mkombozi. Mwalimu wetu ni Bi. Kazamoyo. Yeye huvalia nadhifu kila siku. Pia anapenda kuvaa saa ya dhahabu mkononi. Yeye hubeba kalamu mbili za wino: moja ya kusahihishia madaftari yetu na nyingine ya kuandikia kazi zake. Tunampenda sana Bi. Kazamoyo. Yeye hutufunza kusoma na kuandika kwa njia ya kipekee. Kila mara yeye hutumia chati za hisabati, herufi na maneno na picha kufundishia. Wanafunzi wakisoma vizuri yeye huwatuza kwa wimbo mtamu. Hakuna aliye bora zaidi kuliko Bi. Kazamoyo shuleni Mkombozi.

Siku ya 3

	dh	-ia
	la vu ti a	lavutia
	zi me pambwa zi me bandikwa ku hifadhia	zimepambwa zimebandikwa kuhifadhia
	1. sadara 3. datiwa 5. tibaka	2. kandale 4. buvita

Siku ya 4

	mbw	kw
	Umoja hili ni darasa hili ni dawati hili ni jina hili ni kabati	Wingi haya ni madarasa haya ni madawati haya ni majina haya ni makabati
	darasa	kalenda



Darasa la akina Hamisi

Darasa la akina Hamisi lavutia sana. Yeye na rafiki yake Karani hutumia dawati moja. Kuta za darasa lao zimepambwa kwa chati zenye michoro mizuri. Picha za wanyama na mimea zimebandikwa kwenye kuta hizo. Kuna kabati kubwa la kuhifadhia vitabu vya mwalimu na wanafunzi. Juu ya kabati kuna rejista yenye majina ya wanafunzi wote. Karibu na kabati kuna kalenda ya kuonyesha siku na tarehe.




Siku ya 5

★	th	gh	ng			
☺	m a	ma	a a			
📖	Wakati juzi jana leo kesho kesho kutwa mtondo mtondogoo	Kitenzi walitufunza walitufunza wanatufunza watatufunza watatufunza watatufunza watatufunza				
🏠	ri	ka	ma	ya	a	ze
	mbi	ngo	mba	gi	fi	ta
	kayamba		gitaa			

Maria, Sarun na ala zao za muziki




Siku ya 1

★	dh	sh	-ia
	ki me wa di a i li shu shwa		kimewadia ilishushwa
	ku tu arifu tu li huzunika wa ka kusanyika a li wa aga		kutuarifu. tulihuzunika wakakusanyika aliwaaga
	tulifurahi		walihuzunika

Siku ya 2





	Umoja	Wingi
	mwalimu	walimu
	mwanafunzi	wanafunzi
	mkuu	wakuu
	mgonjwa	wagonjwa
	Umoja	Wingi
	mtu	watu
	mkuu	_____
	_____	walimu
	mgonjwa	_____
_____	wanafunzi	



Darasani

Kengele ilipolia, sote tulifurahi sana. Kipindicha Kiswahili kilikuwa kimewadia. Kila siku mwalimu wa Kiswahili, Bwana Makinda, hutusomea hadithi tamutamu. Siku hiyo Bwana Makinda hakuja. Mwalimu mkuu, Bibi Fahamu, alikuja na kutuarifu kuwa mwalimu wetu ni mgonjwa. Sote tulihuzunika sana. Lakini kiranja wetu, Galana, alijitolea kutusomea hadithi. Hadithi aliyoisoma Galana ilituchekesha sana. Kengele ya pili ilipolia, wanafunzi wote na walimu wakakusanyika mbele ya ofisi ya mwalimu mkuu. Firimbi ilipolia, kila mtu alisimama wima. Bendera ilishushwa. Baadaye, mwalimu mkuu aliwaaga wanafunzi na walimu. Wanafunzi walifurahi mno. Ilikuwa Ijumaa.

Siku ya 3

	dh st kt ng ml mw ia						
	<table style="width: 100%; border: none;"> <tr> <td style="width: 50%;">ma kta ba</td> <td style="width: 50%;">maktaba</td> </tr> <tr> <td>mli ngo ti</td> <td>mlingoti</td> </tr> <tr> <td>mwa nga za</td> <td>mwangaza</td> </tr> </table>	ma kta ba	maktaba	mli ngo ti	mlingoti	mwa nga za	mwangaza
ma kta ba	maktaba						
mli ngo ti	mlingoti						
mwa nga za	mwangaza						
	<table style="width: 100%; border: none;"> <tr> <td style="width: 50%;">kupeperushia</td> <td style="width: 50%;">tulihuzunika</td> </tr> <tr> <td>ilituchekesha</td> <td>wakakusanyika</td> </tr> </table>	kupeperushia	tulihuzunika	ilituchekesha	wakakusanyika		
kupeperushia	tulihuzunika						
ilituchekesha	wakakusanyika						
	<table style="width: 100%; border: none;"> <tr> <td style="width: 50%;">mwangaza</td> <td style="width: 50%;">bustani</td> </tr> </table>	mwangaza	bustani				
mwangaza	bustani						

Siku ya 4

	bw nd ml												
	<table border="1" style="width: 100%; border-collapse: collapse;"> <thead> <tr> <th style="width: 50%; text-align: center;">Umoja</th> <th style="width: 50%; text-align: center;">Wingi</th> </tr> </thead> <tbody> <tr> <td style="text-align: center;">milingoti mrefu</td> <td style="text-align: center;">milingoti mirefu</td> </tr> <tr> <td style="text-align: center;">milingoti mfupi</td> <td style="text-align: center;">milingoti mifupi</td> </tr> <tr> <td style="text-align: center;">milingoti mkubwa</td> <td style="text-align: center;">milingoti mikubwa</td> </tr> <tr> <td style="text-align: center;">milingoti mzuri</td> <td style="text-align: center;">milingoti mizuri</td> </tr> <tr> <td style="text-align: center;">mkebe mweusi</td> <td style="text-align: center;">mikebe mieusi</td> </tr> </tbody> </table>	Umoja	Wingi	milingoti mrefu	milingoti mirefu	milingoti mfupi	milingoti mifupi	milingoti mkubwa	milingoti mikubwa	milingoti mzuri	milingoti mizuri	mkebe mweusi	mikebe mieusi
Umoja	Wingi												
milingoti mrefu	milingoti mirefu												
milingoti mfupi	milingoti mifupi												
milingoti mkubwa	milingoti mikubwa												
milingoti mzuri	milingoti mizuri												
mkebe mweusi	mikebe mieusi												
	<p style="text-align: center;">Jaza pengo</p> <table style="width: 100%; border: none;"> <tr> <td style="width: 50%;">1. p_ndeza</td> <td style="width: 50%;">2. mr_fu</td> </tr> <tr> <td>3. k_bwa</td> <td>4. s_fi</td> </tr> </table>	1. p_ndeza	2. mr_fu	3. k_bwa	4. s_fi								
1. p_ndeza	2. mr_fu												
3. k_bwa	4. s_fi												




Shule ya msingi ya Harambee

Shule ya Msingi ya Harambee ni shule kubwa sana. Ina madarasa makubwa ya mawe. Madarasa haya yana madirisha makubwa ya kuleta mwangaza na hewa safi. Shule ya Harambee ina majengo mengine kama ofisi ya mwalimu mkuu, maktaba na pia chumba cha walimu. Nje ya ofisi ya mwalimu mkuu kuna bustani ya maua ya kupendeza. Katikati ya hii bustani, kuna mlingoti mrefu wa kupandishia na kupeperushia bendera. Shule hii ina uwanja mkubwa sana. Kando ya uwanja huu, kuna vyoo vya wanafunzi na walimu. Wasichana hutumia vyoo tofauti na wavulana. Wanafunzi wanaipenda shule yao.





Siku ya 5

★	ms sh -aa												
🗣️	ku ji ta hi di kujitahidi m si ngi msingi ma shu hu ri mashuhuri ma a di li maadili												
📖	u ta inuka utainuka u ta sifika utasifika												
🏠	<table border="1" style="margin-left: auto; margin-right: auto;"> <tr> <td>sta</td><td>da</td><td>ni</td><td>ma</td><td>u</td><td>sa</td></tr> <tr> <td>ra</td><td>ba</td><td>kta</td><td>wa</td><td>bu</td><td>nja</td></tr> </table> <p style="text-align: center;">maktaba uwanja</p>	sta	da	ni	ma	u	sa	ra	ba	kta	wa	bu	nja
sta	da	ni	ma	u	sa								
ra	ba	kta	wa	bu	nja								




Shule yangu




Siku ya 1

	sh ng md mi mk bw
	u koo ukoo sha nga zi shangazi m ku bwa mkubwa
	a li ni eleza alinieleza ni ta wa ita nitawaita a ka endelea akaendelea
	nyanya amu

Siku ya 2




	a mu amu m jo mba mjomba m do go mdogo															
	<table style="width: 100%; border: none;"> <tr> <td style="width: 33%;"></td> <td style="width: 33%; text-align: center;">(Umoja)</td> <td style="width: 33%; text-align: center;">(Wingi)</td> </tr> <tr> <td>nyanya</td> <td style="text-align: center;">yangu</td> <td style="text-align: center;">yetu</td> </tr> <tr> <td>babu</td> <td style="text-align: center;">yangu</td> <td style="text-align: center;">yetu</td> </tr> <tr> <td>shangazi</td> <td style="text-align: center;">yangu</td> <td style="text-align: center;">yetu</td> </tr> <tr> <td>amu</td> <td style="text-align: center;">yangu</td> <td style="text-align: center;">yetu</td> </tr> </table>		(Umoja)	(Wingi)	nyanya	yangu	yetu	babu	yangu	yetu	shangazi	yangu	yetu	amu	yangu	yetu
	(Umoja)	(Wingi)														
nyanya	yangu	yetu														
babu	yangu	yetu														
shangazi	yangu	yetu														
amu	yangu	yetu														
	<table style="width: 100%; border: none;"> <tr> <td style="width: 50%; text-align: center;">Umoja</td> <td style="width: 50%; text-align: center;">Wingi</td> </tr> <tr> <td style="text-align: center;">1. nyanya yangu</td> <td style="text-align: center;">nyanya yetu</td> </tr> <tr> <td style="text-align: center;">2. dada yangu</td> <td style="text-align: center;">dada yetu</td> </tr> <tr> <td style="text-align: center;">3. mjomba wangu</td> <td style="text-align: center;">_____</td> </tr> <tr> <td style="text-align: center;">4. mtoto wangu</td> <td style="text-align: center;">_____</td> </tr> <tr> <td style="text-align: center;">5. Binamu yangu</td> <td style="text-align: center;">_____</td> </tr> </table>	Umoja	Wingi	1. nyanya yangu	nyanya yetu	2. dada yangu	dada yetu	3. mjomba wangu	_____	4. mtoto wangu	_____	5. Binamu yangu	_____			
Umoja	Wingi															
1. nyanya yangu	nyanya yetu															
2. dada yangu	dada yetu															
3. mjomba wangu	_____															
4. mtoto wangu	_____															
5. Binamu yangu	_____															





Ukoo wetu


Nyanya yangu alinieleza kuhusu ukoo wetu. Aliniambia kuwa yeye na babu yetu walikuwa na watoto watano. Watoto hawa walikuwa Musa, Juma, Paulo, Maria na Jamila. Baba yangu ndiye Juma. Nyanya akanieleza kuwa kaka za baba yangu nitawaita amu. Kwa hivyo, amu zangu ni Musa na Paulo. Pia nyanya akasema kuwa Musa ni baba mkubwa naye Paulo ni baba mdogo. Kwani Musa ni mkubwa wa baba yangu naye Paulo ni mdogo wake. Nyanya akaendelea kusema kuwa Maria na Jamila ni shangazi zangu. Nao watoto wao wote nitawaita binamu. Lakini nyanya akanieleza kuwa kaka ya mama yangu ni mjomba naye dada mkubwa wa mama yangu nitamuita mama mkubwa.

Siku ya 3

	<p>a ja bu ma do a do a vi o ja bwa wa</p>	<p>ajabu madoadoa vioja bwawa</p>
	<p>wa ka m shauri li me toweka pa li kuwa</p>	<p>wakamshauri limetoweka palikuwa</p>
	<p>wabwa mbeng'o</p>	<p>zogam mabo</p> <p>manda</p>

Siku ya 4

	<p>watoto ngo'mbe ngo'mbe ngo'mbe ndama</p>	<p>kumi na wawili wengi mmoja wa ajabu wa madoadoa</p>
	<p>wavulana wanne watoto wengi mtoto mmoja ndama wa ajabu ng'ombe wa madoadoa</p>	



Boma la Wakoli

Mzee Wakoli aliishi kijijini Serere na mke wake pamoja na watoto wao kumi na wawili. Walikuwa na ng'ombe wengi sana. Jioni moja, Mzee Wakoli alikaa na watoto wake na kuwasimulia hadithi. Alisema, siku moja kulikuwa na ng'ombe mmoja aliyezaa ndama wa ajabu. Alikuwa na madoadoa yaliyofanana na ya chui. Jamaa wa Wakoli wakaja kujionea vioja. Wakamshauri Wakoli amuue yule ndama. Wakoli alikataa. Kesho yake wanakijiji wa Serere wakashangaa kuona boma lote la Wakoli limetoweka. Mahala pake palikuwa na bwawa la maji. Tangu siku hiyo, watu wanapomwona ngo'mbe wa madoadoa, humuua mara moja na kutupa mzoga wake msituni.



Siku ya 5

	<p>ku ji ta hi di m si ngi ma shu hu ri ma a di li u ta inuka u ta sifika</p> <p>kujitahidi msingi mashuhuri maadili utainuka utasifika</p>
	<p>ma ja ng'o pa nda mo</p> <p>m s ni ki bo mbe</p> <p>masikini pamoja</p>



Hekima ya mama



Siku ya 1

	ku pu mu li a ku si ki li zi a ku o ne a ku li a ku nywe a ku su gu li a	kupumulia kusikilizia kuonea kulia kunywea kusugulia
	kupumulia	kusikilizia

Siku ya 2

	<table border="1"> <thead> <tr> <th data-bbox="353 923 751 994">Sehemu ya mwili</th> <th data-bbox="751 923 1204 994">Matumizi/kazi yake</th> </tr> </thead> <tbody> <tr> <td data-bbox="353 994 751 1066">macho</td> <td data-bbox="751 994 1204 1066">Kuonea</td> </tr> <tr> <td data-bbox="353 1066 751 1137">Pua</td> <td data-bbox="751 1066 1204 1137">kupumulia</td> </tr> <tr> <td data-bbox="353 1137 751 1209">masikio</td> <td data-bbox="751 1137 1204 1209">kusikilizia</td> </tr> <tr> <td data-bbox="353 1209 751 1280">mdomo</td> <td data-bbox="751 1209 1204 1280">kulia</td> </tr> <tr> <td data-bbox="353 1280 751 1352">mikono</td> <td data-bbox="751 1280 1204 1352">kufanyia kazi</td> </tr> </tbody> </table>		Sehemu ya mwili	Matumizi/kazi yake	macho	Kuonea	Pua	kupumulia	masikio	kusikilizia	mdomo	kulia	mikono	kufanyia kazi
Sehemu ya mwili	Matumizi/kazi yake													
macho	Kuonea													
Pua	kupumulia													
masikio	kusikilizia													
mdomo	kulia													
mikono	kufanyia kazi													
	<p>Sehemu ya mwili na matumizi yake</p> <ol style="list-style-type: none"> 1. pua → kutembelea 2. mguu → kupumulia 3. macho → kulia 4. mdomo → kusikilizia 5. sikio → kuonea 													

Sehemu za mwili

Kila sehemu ya mwili wako ni muhimu na huwa na kazi maalum. Pua hutumiwa kupumulia, masikio kusikilizia na macho kuonea. Mdomo hutumiwa kulia na kunywa, mikono hutumika kufanya kazi mbali mbali. Miguu hutumiwa kumpeleka mtu kokote atakako kwenda. Ni jukumu lako



kuhakikisha kila sehemu ya mwili wako ni safi kuanzia utosini hadi miguuni. Osha kichwa vizuri. Pia hakikisha kipaji, macho, pua na masikio vimeoshwa kwa kutumia kitambaa safi.

Tumia jiwe



maalum kusugua visigino na nyayo. Hakikisha kucha zako zimekatwa vizuri. Ukifanya hivyo, utakuwa na afya bora.



Siku ya 3

	ku ki mu i ka ka ti za ya ka cha ngia	kukimu ikakatiza yakachangia
	I ka katiza ya ka changia	ikakatiza yakachangia


Siku ya 4

	<table border="1"> <thead> <tr> <th></th> <th>Umoja</th> <th>Wingi</th> </tr> </thead> <tbody> <tr> <td></td> <td>mguu</td> <td>miguu</td> </tr> <tr> <td></td> <td>mdomo</td> <td>midomo</td> </tr> <tr> <td></td> <td>mkono</td> <td>mikono</td> </tr> <tr> <td></td> <td>kisogo</td> <td>visogo</td> </tr> <tr> <td></td> <td>kidole</td> <td>vidole</td> </tr> </tbody> </table>			Umoja	Wingi		mguu	miguu		mdomo	midomo		mkono	mikono		kisogo	visogo		kidole	vidole						
	Umoja	Wingi																								
	mguu	miguu																								
	mdomo	midomo																								
	mkono	mikono																								
	kisogo	visogo																								
	kidole	vidole																								
	<table border="1"> <thead> <tr> <th></th> <th>Umoja</th> <th>Wingi</th> </tr> </thead> <tbody> <tr> <td>1.</td> <td>mguu</td> <td>miguu</td> </tr> <tr> <td>2.</td> <td>mdomo</td> <td>midomo</td> </tr> <tr> <td>3.</td> <td>mkono</td> <td>_____</td> </tr> <tr> <td>4.</td> <td>kidole</td> <td>_____</td> </tr> <tr> <td>5.</td> <td>kipaji</td> <td>_____</td> </tr> <tr> <td>6.</td> <td>kisogo</td> <td>_____</td> </tr> <tr> <td>7.</td> <td>jicho</td> <td>_____</td> </tr> </tbody> </table>			Umoja	Wingi	1.	mguu	miguu	2.	mdomo	midomo	3.	mkono	_____	4.	kidole	_____	5.	kipaji	_____	6.	kisogo	_____	7.	jicho	_____
	Umoja	Wingi																								
1.	mguu	miguu																								
2.	mdomo	midomo																								
3.	mkono	_____																								
4.	kidole	_____																								
5.	kipaji	_____																								
6.	kisogo	_____																								
7.	jicho	_____																								




Wanakijiji wa mwili

Wanakijiji wa Mwili walikutana kuzungumzia maisha yao. Mikono ikasema, “Sisi hufanya kazi zote za kukimu mwili.” Miguu ikakatiza, “Nasi huubeba mwili mzima kwenda kokote utakako.”

Macho yakachangia, “Sisi huhitajika kuona wakati wowote kwa hali yoyote.” Masikio yakaongezea, “Nasi huhitajika kusikia chochote wakati wowote kwa hali yoyote.” Mdomo ukasema, “Kwa nini mnadhani ni ninyi peke yenu mnaofanya kazi? Sote tuna kazi maalum: Shingo anaweza kumbeba kichwa. Vidole husaidia Mikono. Kucha husaidia Vidole. Shavu hurembesha uso. Kidevu huwashikilia Mashavu na Mdomo. Wote kijijini Mwili walikubaliana naye.






Siku ya 5

	<p>bi n ti ka s ri m re mbo</p> <p>binti kas ri mrembo</p>												
	<p>a li ye sifika a ta ka ye jibu a ka songea wa li m linda</p> <p>alibesifika atakayejibu akasongea walimlinda</p>												
	<table border="1" data-bbox="418 755 1126 962"> <tr> <td>ma</td> <td>si</td> <td>a</td> <td>do</td> <td>o</td> <td>gu</td> </tr> <tr> <td>mo</td> <td>cho</td> <td>ki</td> <td>pu</td> <td>u</td> <td>m</td> </tr> </table> <p>pua mdomo</p>	ma	si	a	do	o	gu	mo	cho	ki	pu	u	m
ma	si	a	do	o	gu								
mo	cho	ki	pu	u	m								



Binti ya mfalme



Siku ya 1

	sha mba ho da ri ma ku bwa mbe gu n zu ri	shamba hodari makubwa mbegu nzuri
	a li ya uza zi li zo m patia a li tumia	aliyauza zilizompatia alitumia
	mkubwa	zilizompatia

Siku ya 2




	<p style="text-align: center;">Umoja</p>	<p style="text-align: center;">Wingi</p>
	shamba kubwa	mashamba makubwa
	shamba dogo	mashamba madogo
	jembe dogo	majembe madogo
	jembe kubwa	majembe makubwa
	tingatinga dogo	matingatinga madogo
	tingatinga kubwa	matingatinga makubwa
	mashamba matingatinga majembe mashoka mazao	makubwa makubwa _____ _____ _____





Mkulima Hodari

Katika kijiji cha Nguvumali, kulikuwa na mkulima hodari sana. Aliitwa Mzee Bidii. Yeye alikuwa na mashamba makubwa na madogo. Alipotaka kulima shamba dogo alitumia kifyekeo kukata nyasi, kisha akalima kwa jembe. Kama shamba lilikuwa kubwa, alitumia shoka kukatia miti mikubwa. Pia aling'oa mizizi ya miti kwa uma. Baadaye alitumia trekta au tingatinga kulima shamba hilo. Alipanda mbegu nzuri zilizompatia mazao mengi. Aliyauza mazao hayo na kuwa tajiri.

Siku ya 3

	ki bi na fsi fe dha	kibinafsi fedha	
	I na yo pandwa u ku lima	inayopandwa ukulima	
	ga mbo ndi ma hi	zi a vi go ho mi	zi ndi

Siku ya 4




	Umoja	Wingi
	ukulima wangu	ukulima wetu
	mmea wangu	mmea wetu
	matumizi yangu	matumizi yetu
	ukulima wako	ukulima wenu
	mmea wako	mmea wenu
	matumizi yako	matumizi yenu
	ukulima wake	ukulima wao
	mmea wake	mmea wao
	matumizi yake	matumizi yao
	1. baadhi 3. fedha 5. inayopandwa	2. kibinafsi 4. ukulima



Ukulima

Ukulima ni kazi muhimu sana kwa ufanisi wa nchi. Kuna aina mbili za wakulima. Baadhi ya wakulima hulima ili wapate mazao kwa matumizi yao ya kibinafsi. Wakulima wengine hulima ili wauze mazao na kupata fedha. Mimea inayopandwa kwa matumizi ya nyumbani ni kama vile: mahindi, mboga, mihogo, ndizi na viazi vitamu. Mimea inayopandwa kwa ajili ya kuuza ni kama vile: kahawa, maua na majani chai.




Siku ya 5

	<p>ha u o zi ha ku ju a wa na o ni ku ga wi e</p>	<p>hauzi hakujua wanao nikugawie</p>												
	<p>ha ku jua ki ka m shukuru ki ka m shauri</p>	<p>hakujua kikamshukuru kikamshauri</p>												
	<table border="1" style="margin-left: auto; margin-right: auto;"> <tr> <td style="background-color: #333; color: white; padding: 5px;">wa</td> <td style="background-color: #333; color: white; padding: 5px;">e</td> <td style="background-color: #333; color: white; padding: 5px;">mu</td> <td style="background-color: #333; color: white; padding: 5px;">ma</td> <td style="background-color: #333; color: white; padding: 5px;">m</td> <td style="background-color: #333; color: white; padding: 5px;">ki</td> </tr> <tr> <td style="background-color: #333; color: white; padding: 5px;">ze</td> <td style="background-color: #333; color: white; padding: 5px;">na</td> <td style="background-color: #333; color: white; padding: 5px;">ke</td> <td style="background-color: #333; color: white; padding: 5px;">ki</td> <td style="background-color: #333; color: white; padding: 5px;">me</td> <td style="background-color: #333; color: white; padding: 5px;">ja</td> </tr> </table> <p style="text-align: center;">mume</p>		wa	e	mu	ma	m	ki	ze	na	ke	ki	me	ja
wa	e	mu	ma	m	ki									
ze	na	ke	ki	me	ja									




Wema hauzi




Siku ya 1

	<p>wa na m ju a hu fa na ni shwa u ha ri bi fu ki chu gu u zi li zo m patia</p>	<p>wanamjua hufananishwa uharibifu kichuguu zilizompatia</p>
	<ol style="list-style-type: none"> 1. Mchwa walikula na kuharibu mlango wa nyumba yetu. 2. Mkulima aliweka mahindi ghalani. 	
	wanamjua	hufananishwa


Siku ya 2

	<p>mazao yake nyumba yake miti yake</p>	<p>bidii yake sifa yake kazi yake</p>
	<ol style="list-style-type: none"> 1. Mchwa ana sifa nzuri kutokana na bidii yake. 2. Mchwa hujenga nyumba yake kwa mate 	
	<p>uhar_bifu m_te</p>	<p>b_dii s_fa ny_mba</p>



Mchwa




Mchwa ni mdudu ambaye ana sifa nyingi. Watu wanamjua mchwa kwa uharibifu wake. Kwa mfano anaweza kuharibu mazao ghalani na kula miti na vigingi vya nyumba. Mbali na uharibifu, mchwa ana sifa nzuri kutokana na bidii yake. Je, wajuu kwamba mchwa hujenga nyumba yake kwa mate? Nyumba hii huitwa kichuguu. Watu wanaofanya kazi kwa bidii hufananishwa na mchwa. Watu wanaofanya kazi kwa bidii kama mchwa hufanikiwa.




Sherehe ya wadudu

Katika shamba la Ngomeni kulizuka vita vikali. Vita hivyo vilikuwa baina ya kombamwiko na kiwavi. Kombamwiko alikuwa amechafua vazi la kiwavi ambalo huwa maridadi sana. Ni lazima kuwe na mapatano! Kiroboto aliwaza. Aliona ni heri aandae sherehe na kuwaalika wadudu wote. Kiroboto alifanya hivyo. Ilopowadia mwendo wa saa nne, wadudu walianza kuingia. Waliohudhuria walikuwa kiwavi, nyuki, nzi, panzi, na kumbikumbi. Konokono akaamua kwenda kwenye sherehe ijapokuwa yeye si mdudu. Alipokuwa njiani kuelekea huko, aliumwa na siafu. Akakimbizwa katika zahanati. Wadudu wakala vyakula na kunywa vinywaji. Mwishowe wakasameheana. Wadudu wakaishi raha mustarehe.




Siku ya 5

	<p>vi pe pe o ko mba mwi ko chu ngu m cha nga ni ja ngwa ni</p>	<p>vipepeo kombamwiko chungu mchangani jangwani</p>												
	<p>wa na o patikana i me gawanyika i ja po kuwa wa na weza</p>	<p>wanaopatikana imegawanyika ijapokuwa wanaweza</p>												
	<table border="1" style="width: 100%; text-align: center;"> <tr> <td style="background-color: #333; color: white; padding: 5px;">vi</td> <td style="background-color: #333; color: white; padding: 5px;">nyu</td> <td style="background-color: #333; color: white; padding: 5px;">si</td> <td style="background-color: #333; color: white; padding: 5px;">gu</td> <td style="background-color: #333; color: white; padding: 5px;">pe</td> <td style="background-color: #333; color: white; padding: 5px;">n</td> </tr> <tr> <td style="background-color: #333; color: white; padding: 5px;">chu</td> <td style="background-color: #333; color: white; padding: 5px;">o</td> <td style="background-color: #333; color: white; padding: 5px;">ngu</td> <td style="background-color: #333; color: white; padding: 5px;">zi</td> <td style="background-color: #333; color: white; padding: 5px;">nyi</td> <td style="background-color: #333; color: white; padding: 5px;">ki</td> </tr> </table> <p style="text-align: center; margin-top: 10px;">nzi nyigu</p>		vi	nyu	si	gu	pe	n	chu	o	ngu	zi	nyi	ki
vi	nyu	si	gu	pe	n									
chu	o	ngu	zi	nyi	ki									




Wadudu



Siku ya 1

	ma wi ngu a nga ni mbi ngu mi ngu ru mo m vu a	mawingu angani mbingu mingurumo mvua
	tu ki rukaruka i ka badilika ya ka tanda u nge dhani zi me toboka	tukirukaruka ikabadilika yakatanda ungedhani zimetoboka
	mawingu mwangaza	


Siku ya 2

	<table border="1"> <tr> <td data-bbox="337 948 718 1023">tukaona</td> <td data-bbox="718 948 1100 1023">hatukuona</td> </tr> <tr> <td data-bbox="337 1023 718 1099">tukasikia</td> <td data-bbox="718 1023 1100 1099">hatukusikia</td> </tr> <tr> <td data-bbox="337 1099 718 1174">tukarudi</td> <td data-bbox="718 1099 1100 1174">hatukurudi</td> </tr> <tr> <td data-bbox="337 1174 718 1250">tukacheza</td> <td data-bbox="718 1174 1100 1250">hatukucheza</td> </tr> <tr> <td data-bbox="337 1250 718 1325">tukatoroka</td> <td data-bbox="718 1250 1100 1325">hatukutoroka</td> </tr> </table>		tukaona	hatukuona	tukasikia	hatukusikia	tukarudi	hatukurudi	tukacheza	hatukucheza	tukatoroka	hatukutoroka
tukaona	hatukuona											
tukasikia	hatukusikia											
tukarudi	hatukurudi											
tukacheza	hatukucheza											
tukatoroka	hatukutoroka											
	1. Mawingu meusi yalitanda angani 2. Mvua iliponyesha tulisikia migurumo ya radi											
	<table border="1"> <tr> <td data-bbox="337 1483 692 1559">tulirukaruka</td> <td data-bbox="692 1483 1109 1559">hatukurukaruka</td> </tr> <tr> <td data-bbox="337 1559 692 1634">ikabadilika</td> <td data-bbox="692 1559 1109 1634">_____</td> </tr> <tr> <td data-bbox="337 1634 692 1709">zilionekana</td> <td data-bbox="692 1634 1109 1709">_____</td> </tr> <tr> <td data-bbox="337 1709 692 1785">zilitoboka</td> <td data-bbox="692 1709 1109 1785">_____</td> </tr> </table>		tulirukaruka	hatukurukaruka	ikabadilika	_____	zilionekana	_____	zilitoboka	_____		
tulirukaruka	hatukurukaruka											
ikabadilika	_____											
zilionekana	_____											
zilitoboka	_____											



Anga




Hali ya anga ilikuwa tulivu. Tulikuwa uwanjani tukirukaruka kama vipepeo. Mara hali ya hewa ikabadilika. Mawingu meusi yakatanda angani. Mbingu zilionekana kama zilizofunikwa kwa blanketi jeusi. Muda mchache baadaye, tukaona mwangaza mkali. Kisha tukasikia mingurumo ya radi. Kwa woga sote tulitorokea darasani. Punde si punde, mvua nyingi ikaanza kunyesha. Ungedhani mbingu zimetoboka. Mvua ilipopungua sote tulirudi uwanjani tukacheza kwa maji ya mvua.




Mvua

Mvua hutokana na maji yaliyoko angani. Wakati kuna jua kali, maji huyeyuka angani. Maji haya hukusanyika na kuwa matone. Matone haya ya maji yanapokusanyika, huwa tunaona mawingu meusi. Haya mawingu huwa yamebeba matone mengi ya maji. Matone haya yanapokuwa mazito, huwa yanaanguka. Ndipo tunaona mvua ikinyesha. Mvua inaponyesha, mimea hufurahia kwani inapata maji na kunawiri. Mito pia hufurahia maji ya mvua. Watu nao pia hufurahia sana.



Siku ya 5

	Umoja	Wingi				
	mwanadamu yuko wapi?	wanadamu wako wapi?				
	mnyama yuko wapi?	wanyama wako wapi?				
	mdudu yuko wapi?	wadudu wako wapi?				
	Ramani ya hadithi					
	pi	ku	o	sa	sha	ka
	fu	ga	nywa	fi	a	ni
kusafisha						

Maji



Siku ya 1

★	a	-aa	-ee	-ei	-eo
	-ia	ie	-io	o	u
	-uo	ch	dh	n	nd
	m	ng	sh	tw	w
	te	kno	lo	ji	a
	ta	ra	ki	li	shi
	te	le	vi	she	ni
	ru	nu	nu		
		bei		dhiki	

Teknolojia

Dunia imebadilika, teknolojia imeingia
Bara, pwani imefika, wote wameitikia

Redio nazo tunazo, nyumbani na kwenye simu
Mawaidha na vitulizo, mafundisho yakuheshimu

Tarakilishi twatumia, shuleni hata
kazini
Zina michezo ya kuvutia, zitumie kwa
makini.

Runinga zimeenea, zaitwa televisheni
Picha video kuonea, muziki pia sikizeni

Simu zimetapakaa, kila pahali nchini
Za rununu na za waya, twatuma hata matini



Siku ya 2




★	E e -ao ch mv	H h -eo dh nj	I i -eu mch ny	S s -ia mw	B kw mk	-aa bl nd
	zi li o ne ka na zi li zo fu ni kwa tu li to ro ke a zi me to bo ka			zilionekana zilizofunikwa tulitorokea zimetoboka		
	vipepeo mawingu		yakatanda mwangaza	mingurumo		
	mbao		nyika			

Anga



Hali ya anga ilikuwa tulivu. Tulikuwa uwanjani tukirukaruka kama vipepeo. Mara hali ya hewa ikabadilika. Mawingu meusi yakatanda angani. Mbingu zilionekana kama zilizofunikwa kwa blanketi jeusi. Muda mchache baadaye, tukaona mwangaza mkali. Kisha tukasikia mingurumo ya radi. Kwa woga sote tulitorokea darasani. Punde si punde, mvua nyingi ikaanza kunyesha. Ungedhani mbingu zimetoboka. Mvua ilipopusa sote tulirudi uwanjani tukacheza kwa maji ya mvua.

Siku ya 3

	che ndo	ga ngi	hi sho	nchu sta	mbe
		u hu nzi so na ra dha ha bu ba ngi li		uhunzi sonara dhahabu bangili	
	a na tengeneza hu tengeneza tu na weza ku ji ajiri			anatengeneza hutengeneza tunaweza kujiajiri	

Mzee Kibyego




Mzee Kibyego hufanya kazi ya uhunzi. Yeye ni mhunzi. Anatengeneza vitu kama karai, sufuria na majiko kwa kutumia vyuma.

Kazi hii inahitaji nguvu nyingi na uvumilivu. Mhunzi ni lazima atumie ujuzi mwingi


kabisa. Mke wa Kibyego ni Sonara. Yeye hutengeneza vitu vya dhahabu – kama pete, vipuli na bangili. Mzee Kibyego na mke wake hupata pesa nyingi sana.

Siku hizi ni vigumu kupata kazi za ofisi. Tunaweza kutumia ujuzi wetu kujiajiri wenyewe kama mzee Kibyego na mke wake.

Siku ya 4

	m k a mka m p e mpe nj w a njwa k t a kta mb u mbu ng a nga	m w i mwi s p i spi k w e kwe t w a twa m f a mfa m w o mwo
	mwi li mwili da k ta ri daktari	ma ra dhi maradhi u go njwa ugonjwa
	a ki tetemeka u na o letwa	akitetemeka unaoletwa
	alimshauri	akamwambia

Ugonjwa wa malaria





Tumaini aliamka akiwa anatetemeka mwili. Mwili wake ulikuwa na joto kali. Mama yake akaamua kumpeleka hospitali ya Shauri Moyo.

Hospitalini kulikuwa na wagonjwa wengi wenye maradhi

tofauti tofauti. Magonjwa kama vile homa, kikohozi, upele, malaria. Wote walikuwa wameketi kwenye fomu wakingoja kumwona daktari.

Baada ya mda Daktari akamwita kwenye chumba na kumfanyia uchunguzi. Hapo ndipo alimueleza kuwa alikuwa na ugonjwa wa malaria. Huu ni ugonjwa unaoletwa na mbu. Ili kujikinga na magonjwa haya tunafaa kuhakikisha mbu hawazaani karibu na nyumba zetu.





Siku ya 5

★	<p>b w a bwa</p> <p>m b e mbe</p> <p>n n e nne</p>	<p>m w a mwa</p> <p>s h i shi</p> <p>m f a mfa</p>
	<p>ki u</p> <p>mi nne</p> <p>ki vu li</p> <p>na zaa</p>	<p>kiu</p> <p>minne</p> <p>kivuli</p> <p>nazaa</p>
	<div style="display: flex; flex-wrap: wrap; justify-content: space-around;"> <div style="background-color: #333; color: white; padding: 5px; margin: 2px;">pi</div> <div style="background-color: #333; color: white; padding: 5px; margin: 2px;">ku</div> <div style="background-color: #333; color: white; padding: 5px; margin: 2px;">o</div> <div style="background-color: #333; color: white; padding: 5px; margin: 2px;">sa</div> <div style="background-color: #333; color: white; padding: 5px; margin: 2px;">sha</div> <div style="background-color: #333; color: white; padding: 5px; margin: 2px;">ka</div> <div style="background-color: #333; color: white; padding: 5px; margin: 2px;">fu</div> <div style="background-color: #333; color: white; padding: 5px; margin: 2px;">ga</div> <div style="background-color: #333; color: white; padding: 5px; margin: 2px;">nywa</div> <div style="background-color: #333; color: white; padding: 5px; margin: 2px;">ki</div> <div style="background-color: #333; color: white; padding: 5px; margin: 2px;">bo</div> <div style="background-color: #333; color: white; padding: 5px; margin: 2px;">mbe</div> </div> <p style="text-align: center;">kia kivuli</p>	




Maji




Siku ya 1

	dh a dha z w a zwa z w i zwi nd w i ndwi dh u dhu
	dhu lu ma dhuluma ku mu a dhi bu kumuadhibu ku si ki zwa kusikizwa ku li ndwa kulindwa ku fu ra hi a kufurahia
	i na m linda inamlinda wa na zo ruhusiwa wanazoruhusiwa
	dhuluma kusikizwa

Siku ya 2




	dh u dhu z w i zwi nd w a ndwa								
	<table border="1" data-bbox="445 1323 1029 1613"> <tr> <td>shule</td> <td>shuleni</td> </tr> <tr> <td>kazi</td> <td>kazini</td> </tr> <tr> <td>nyumba</td> <td>nyumbani</td> </tr> <tr> <td>mchezo</td> <td>mchezoni</td> </tr> </table>	shule	shuleni	kazi	kazini	nyumba	nyumbani	mchezo	mchezoni
shule	shuleni								
kazi	kazini								
nyumba	nyumbani								
mchezo	mchezoni								
	1. kutibu _____ 2. kuchapa _____ 3. kucheza _____								






Haki za watoto

Katiba ya Kenya inamlinda mtoto kutokana na dhuluma za kila aina. Kila mtoto ambaye amefikisha umri wa miaka sita anapaswa kuwa shuleni. Watoto hawaruhusiwi kufanya kazi ya kulipwa. Watoto wanapaswa kufanya kazi za kusaidia wazazi nyumbani. Ni hatia kwa mtu yeyote kumuadhibu mtoto kwa kumchapa. Watoto pia wana haki ya kulindwa, kupata matibabu yanayofaa na haki ya kusikizwa. Ni haki ya watoto kucheza na kufurahia maisha yao.

Siku ya 3

	ma gu ru du mu	magurudumu
	wa na o zaliwa ki maumbile hu chechemea tu na faa ku wa saidia ku to ji weza	wanaozaliwa kimaumbile huchechemea tunafaa kuwasaidia kutojiweza
	walemavu	kimaumbile

Siku ya 4



pinde	6	sita																							
nyanja	6	sita																							

	rangi	1	(moja)
	rangi	2	(mbili)
	rangi	3	(tatu)
	rangi	_____	nne
	rangi	5	_____
	rangi	_____	sita
	rangi	7	_____
	rangi	_____	nane
	rangi	9	_____
	rangi	_____	kumi




Upinde wa mvua





Upinde wa mvua una rangi saba za kupendeza. Jua linapomulika mwangaza kwenye matone ya maji ndipo upinde wa mvua hupatikana. Upinde wa mvua huonekana wakati wa mchana. Mwangaza

wa jua huwa na rangi nyeupe tu. Ni wakati unapokutana na matone ya maji ndipo rangi hutawanyika. Rangi ya kwanza ni nyekundu. Ya pili ni rangi ya machungwa na ya tatu ni rangi ya manjano. Rangi zingine ni rangi ya kijani kibichi, samawati, nili ama indigo na rangi ya urujuani.

Siku ya 5

	<table border="1"> <thead> <tr> <th data-bbox="395 359 728 432">Neno</th> <th data-bbox="728 359 1144 432">Hali ya Kukanusha</th> </tr> </thead> <tbody> <tr> <td data-bbox="395 432 728 506">yalipoteza</td> <td data-bbox="728 432 1144 506">hayakupoteza</td> </tr> <tr> <td data-bbox="395 506 728 579">yalitapakaa</td> <td data-bbox="728 506 1144 579">hayakutapakaa</td> </tr> <tr> <td data-bbox="395 579 728 653">yalisababisha</td> <td data-bbox="728 579 1144 653">hayakusababisha</td> </tr> <tr> <td data-bbox="395 653 728 726">yalionekana</td> <td data-bbox="728 653 1144 726">hayakuonekana</td> </tr> </tbody> </table>		Neno	Hali ya Kukanusha	yalipoteza	hayakupoteza	yalitapakaa	hayakutapakaa	yalisababisha	hayakusababisha	yalionekana	hayakuonekana		
Neno	Hali ya Kukanusha													
yalipoteza	hayakupoteza													
yalitapakaa	hayakutapakaa													
yalisababisha	hayakusababisha													
yalionekana	hayakuonekana													
	<table> <tr> <td data-bbox="443 797 621 846">kitambo</td> <td data-bbox="852 797 985 846">kidogo</td> </tr> <tr> <td data-bbox="443 852 621 900">mafuriko</td> <td data-bbox="852 852 1002 900">gharika</td> </tr> <tr> <td data-bbox="443 906 563 954">safina</td> <td data-bbox="852 906 1103 954">waliangamia</td> </tr> <tr> <td data-bbox="443 960 694 1008">waling'amua</td> <td></td> </tr> </table>		kitambo	kidogo	mafuriko	gharika	safina	waliangamia	waling'amua					
kitambo	kidogo													
mafuriko	gharika													
safina	waliangamia													
waling'amua														
	<table border="1"> <thead> <tr> <th data-bbox="395 1051 797 1124">Halisi</th> <th data-bbox="797 1051 1144 1124">Kukanusha</th> </tr> </thead> <tbody> <tr> <td data-bbox="395 1124 797 1197">Waliwaza</td> <td data-bbox="797 1124 1144 1197">Hawakuwaza</td> </tr> <tr> <td data-bbox="395 1197 797 1271">Walisema</td> <td data-bbox="797 1197 1144 1271"></td> </tr> <tr> <td data-bbox="395 1271 797 1344">Waliogelea</td> <td data-bbox="797 1271 1144 1344"></td> </tr> <tr> <td data-bbox="395 1344 797 1418">Walipoteza</td> <td data-bbox="797 1344 1144 1418"></td> </tr> <tr> <td data-bbox="395 1418 797 1491">Walitamani</td> <td data-bbox="797 1418 1144 1491"></td> </tr> </tbody> </table>		Halisi	Kukanusha	Waliwaza	Hawakuwaza	Walisema		Waliogelea		Walipoteza		Walitamani	
Halisi	Kukanusha													
Waliwaza	Hawakuwaza													
Walisema														
Waliogelea														
Walipoteza														
Walitamani														

Siku la 1

	<p>cho mbo ki sa sa mu da wa ka ti sa a ma u mbo shu ghu li</p>	<p>chombo kisasa muda wakati saa maumbo shughuli</p>
	<p>i na m linda wa na zo ruhusiwa hu to fautiana ku to chelewa</p>	<p>inamlinda wanazoruhusiwa hutofautiana kutochelewa</p>


Siku la 2

	<table border="1"> <thead> <tr> <th data-bbox="454 1340 765 1412">Umoja</th> <th data-bbox="765 1340 1104 1412">Wingi</th> </tr> </thead> <tbody> <tr> <td data-bbox="454 1412 765 1483">saa hii</td> <td data-bbox="765 1412 1104 1483">saa hizi</td> </tr> <tr> <td data-bbox="454 1483 765 1555">ofisi hii</td> <td data-bbox="765 1483 1104 1555">ofisi hizi</td> </tr> <tr> <td data-bbox="454 1555 765 1626">nyumba hii</td> <td data-bbox="765 1555 1104 1626">nyumba hizi</td> </tr> <tr> <td data-bbox="454 1626 765 1698">hospitali hii</td> <td data-bbox="765 1626 1104 1698">hospitali hizi</td> </tr> </tbody> </table>		Umoja	Wingi	saa hii	saa hizi	ofisi hii	ofisi hizi	nyumba hii	nyumba hizi	hospitali hii	hospitali hizi
Umoja	Wingi											
saa hii	saa hizi											
ofisi hii	ofisi hizi											
nyumba hii	nyumba hizi											
hospitali hii	hospitali hizi											

Saa

Saa ni chombo cha kisasa cha kupimia muda au wakati. Kuna saa za kufungwa mkononi. Hizi huwa ndogo kiasi lakini hutofautiana kwa maumbo na ukubwa wake. Kuna saa za kuwekwa au kutundikwa ukutani.

Hizi nazo hutofautiana kwa maumbo na ukubwa wake. Pia kuna saa za kuwekwa mezani. Hizi pia hutofautiana kwa maumbo na ukubwa wake. Saa za mkono mara nyingi hutumiwa na mtu mmoja. Saa za ukutani na mezani mara nyingi hutumiwa na watu wengi. Saa ni muhimu shuleni, ofisini, nyumbani na hata hospitalini. Ni vizuri kuwa na saa. Itakusadia kutochelewa kwa shughuli zako za kila siku.




Siku la 3

★	hu ru di hurudi wa ka ti wakati hu a nza huanza
🗣️	pa re di paredi fo le ni foleni
📖	i na po wadia inapowaida hu wa ongoza huwaongoza ku poteza kupoteza hu ji tayarisha hujitayarisha

Siku la 4




🗣️	<p>Mwema huishi karibu na shule. Mwema huamka asubuhi na mapema. Mwema hupata kiamsha kinywa. Mwema huanza safari ya kwenda shule. Mwema hupanga foleni ya kwenda paredi. Mwema hurudi nyumbani. Mwema huimba wimbo “nasikia sauti”.</p>
----	--



Mwema

Mwema huishi karibu na shule yake. Yeye huamka saa kumi na mbili za asubuhi. Bila kupoteza wakati yeye hujitayarisha kwenda shule. Saa moja inapowadia, Mwema hupata kiamsha kinywa. Kisha yeye huanza safari yake kwenda shuleni. Saa mbili wanafunzi hupanga foleni kwenda paredi. Baada ya paredi wanafunzi hurudi darasani kuanza masomo. Saa nne kamili wao huenda kucheza nje na marafiki zao. Saa sita kamili, Mwema hurudi nyumbani. Kabla ya kwenda, mwalimu wao huwaongoza kuimba wimbo mtamu wa “Nasikia Sauti.”



Siku la 5

	kasuku	kujipachika	alimaka
	u li po wadia a li yo ya sema ya li yo tendeka wa li geuka	ulipowadia alivyosema yaliyotendeka waligeuka	
	Mchoro wa saa		



Obura na saa yake




Siku ya 1

	<table border="0"> <tr> <td data-bbox="422 343 738 546"> ku pe nde za mbu ga ma zi ngi ra ma a ja bu </td> <td data-bbox="852 343 1067 546"> kupendeza mbuga mazingira maajabu </td> </tr> </table>	ku pe nde za mbu ga ma zi ngi ra ma a ja bu	kupendeza mbuga mazingira maajabu								
ku pe nde za mbu ga ma zi ngi ra ma a ja bu	kupendeza mbuga mazingira maajabu										
	<table border="1"> <thead> <tr> <th data-bbox="412 620 776 691">Umoja</th> <th data-bbox="776 620 1129 691">Wingi</th> </tr> </thead> <tbody> <tr> <td data-bbox="412 691 776 765">anapofikiria</td> <td data-bbox="776 691 1129 765">wanapofikiria</td> </tr> <tr> <td data-bbox="412 765 776 838">anapotuletea</td> <td data-bbox="776 765 1129 838">wanapotuletea</td> </tr> <tr> <td data-bbox="412 838 776 911">anaposifika</td> <td data-bbox="776 838 1129 911">wanaposifika</td> </tr> <tr> <td data-bbox="412 911 776 985">anapotafuta</td> <td data-bbox="776 911 1129 985">wanapotafuta</td> </tr> </tbody> </table>	Umoja	Wingi	anapofikiria	wanapofikiria	anapotuletea	wanapotuletea	anaposifika	wanaposifika	anapotafuta	wanapotafuta
Umoja	Wingi										
anapofikiria	wanapofikiria										
anapotuletea	wanapotuletea										
anaposifika	wanaposifika										
anapotafuta	wanapotafuta										

Siku ya 2




	<table border="1"> <tr> <td data-bbox="378 1155 755 1244">wanariadha wetu</td> <td data-bbox="755 1155 1163 1244">wanariadha wenu</td> </tr> <tr> <td data-bbox="378 1244 755 1333">wanyama wetu</td> <td data-bbox="755 1244 1163 1333">wanyama wenu</td> </tr> <tr> <td data-bbox="378 1333 755 1421">watu wetu</td> <td data-bbox="755 1333 1163 1421">watu wenu</td> </tr> </table>	wanariadha wetu	wanariadha wenu	wanyama wetu	wanyama wenu	watu wetu	watu wenu
wanariadha wetu	wanariadha wenu						
wanyama wetu	wanyama wenu						
watu wetu	watu wenu						
	<table border="1"> <tr> <td data-bbox="378 1483 772 1566">watu wetu</td> <td data-bbox="772 1483 1166 1566">watu wao</td> </tr> <tr> <td data-bbox="378 1566 772 1649">wanariadha wetu</td> <td data-bbox="772 1566 1166 1649">_____</td> </tr> <tr> <td data-bbox="378 1649 772 1733">wanyama wetu</td> <td data-bbox="772 1649 1166 1733">_____</td> </tr> </table>	watu wetu	watu wao	wanariadha wetu	_____	wanyama wetu	_____
watu wetu	watu wao						
wanariadha wetu	_____						
wanyama wetu	_____						





Nchi ya Kenya

Kenya ni nchi ya kupendeza sana. Watu wengi hufurahia kuzuru Kenya kuliko nchi nyingine yoyote Barani Afrika. Wanariadha wetu wametuletea sifa ulimwenguni kwa ushindi wao katika mbio za masafa marefu. Watu kutoka bara zingine huja kuwaona wanyama wa porini kwenye mbuga zetu. Mji wa Nairobi ni mji wa pekee ambao una mbuga ya wanyama barani Afrika. Mlima Kenya unasifika kama mlima wa pili kwa urefu katika bara la Afrika. Mbuga ya Masai Mara ni moja kati ya maajabu saba ya dunia. Hii ni kwa sababu ya kongoni na wanyama wengine ambao huvuka mto Serengeti na mto Mara katika msimu wao kila mwaka. Ni desturi kwa wanyama hawa huvuka kuja upande wa Kenya au kwenda upande wa Tanzania kutafuta malisho. Wanyama wanahitaji mazingira mema. Ili tunufaike na utalii ni lazima tulinde mazingira yetu.

Siku ya 3

	haviozi huboresha	tukome mmomonyokoe	changamoto
	tu na vyo tumia hu te nge nezwa vi na po tupwa vi li vyo tengenezwa	tunavyotumia hutengenezwa vinapotupwa vilivyotengenezwa	
	Sentensi		Kukanusha
	Vitu vinaoza .		Vitu haviozi .
	vyuma vinatumiwa .		
	vitabu vinaruhusiwa .		
	vitu vinarushwa .		

Siku ya 4



	kuleta	kutoleta		
	kuyalinda	kutoyalinda		
	kupunguza	kutopunguza		
	kurusha	kutorusha		
	kupanda	kutopanda		
	kuathiri	kutoathiri		
	Vyombo vya chuma	Vyombo vya mbao	Vyombo vya karatasi	Vyombo vya plastiki



Linda Mazingira Yetu

Vitu vingi tunavyotumia kila siku hutengenezwa kwa vyuma, mbao, plastiki au hata chupa. Vitu hivi vinapotupwa, haviози kwa urahisi. Hivyo basi changamoto kubwa tuliyo nayo ni jinsi ya kutumia vitu hivyo kwa njia isiyothiri vibaya mazingira yetu. Lazima turushe takataka mahali panapofaa. Ni vyema pia kutumia vitu vilivyotengenezwa kwa chupa, karatasi, chuma au plastiki kwa muda mrefu kabla ya kuvitupa. Hatuna budi kupanda miti mingi kadri ya uwezo wetu. Miti huboresha hali ya hewa, hupunguza mmomonyoko wa udongo na kuleta mvua. Ni wajibu wetu kuyalinda mazingira yetu kwa ajili yetu na vizazi vijavyo.



Siku ya 5

	<p>m go mba u ki e le a u ki ngo ni wa nge ga wa na ku chu ma ma ga nda ki na</p> <p>mgomba ukielea ukingoni wangepawana kuchuma maganda kina</p>
	<p>Mbali na shule Chini ya meza Juu ya _____ Kando ya _____ Karibu na _____</p>



Kobe na nyani



Siku ya 1

	ma pa cha a fu e ni i ta ki ka na vyo u gu a	mapacha afueni itakikanavyo ugua
	si ji wezi si ji tambui	sijiwezi sijitambui

Siku ya 2

	<p style="text-align: center;">Halisi</p>	<p style="text-align: center;">Kukanusha</p>
	<p>Nitaumwa.</p>	<p>Sitaumwa.</p>
	<p>Nitabaki.</p>	<p>Sitabaki.</p>
	<p>Nitamsaidia.</p>	<p>Sitamsaidia.</p>
	<p>Nitapiga.</p>	<p>Sitapiga.</p>
	<p>Nitakuwa.</p>	<p>Sitakuwa.</p>
	<p>Nitampeleka.</p>	<p>Sitampeleka.</p>
	<p style="text-align: center;">Halisi</p>	<p style="text-align: center;">Kukanusha</p>
	<p>Nitaumwa sana.</p>	<p>Sitaumwa sana</p>
	<p>Nitabaki hapa nyumbani.</p>	<p>_____</p>
	<p>Nitamsaidia mama yako.</p>	<p>_____</p>
	<p>Nitapiga simu kazini.</p>	<p>_____</p>
	<p>Nitakuwa mgonjwa.</p> <p>Nitampeleka mama hospitalini.</p>	<p>_____</p>

Mchezo wa Kuigiza: Mama Augua



Msimulizi: Hapo zamani za kale paliishi baba, mama na watoto wao mapacha. Msichana aliitwa Maria na mvulana aliitwa Matano. Mapacha hao walikuwa na miaka saba na walikuwa katika darasa la pili. Siku moja mama akawa mgonjwa.

Mama: Wanangu, naumwa sana. Sijiwezi sijitambui. Inabidi niende kumwona daktari mara moja. Baba yenu atanipeleka.



Baba: Hapana! Ni lazima niende kazini! Nyote mwanitegemea kwa hali na mali. Kila mara mama ananiomba pesa za matumizi ya hapa nyumbani. Maria, hauendi shuleni leo. Utabaki hapa nyumbani umsaidie mamako. Pia utaenda kutafuta kuni, kuchota maji na kupika chakula. Na Matano, utampeleka mamako hospitalini.

Maria: Lakini baba tusipoenda shule tutaachwa nyuma kimasiku. Tafadhali baba turuhusu tuende. Wewe ni mkubwa kuliko sisi. Ni wajibu wako kumpeleka mama hospitalini. Pia unaweza kumsaidia vyema kuliko sisi.



Baba: Ninaona mnapenda kusoma sana wanangu. Haya basi, nendeni. Hebu nami nipige simu kazini kuomba ruhusa kumpeleka mama yenu hospitalini na kumtunza itakikanavyo.


Matano: Ahsante, baba. Naamini mama atapata afueni.

Siku ya 3

	<p>ka ti ba po to vu ka ba mbe ka nu ni ma dha ra hu si ka</p>	<p>katiba potovu kabambe kanuni madhara husika</p>
	<p>zi na zo tokana ku wa saidia</p>	<p>zinazotokana kuwasaidia</p>

Siku ya 4


	<table border="1"> <thead> <tr> <th data-bbox="340 855 749 929">Neno</th> <th data-bbox="749 855 1153 929">Kinyume</th> </tr> </thead> <tbody> <tr> <td data-bbox="340 929 749 1006">mila nzuri</td> <td data-bbox="749 929 1153 1006">mila potovu</td> </tr> <tr> <td data-bbox="340 1006 749 1083">bahati nzuri</td> <td data-bbox="749 1006 1153 1083">bahati mbaya</td> </tr> <tr> <td data-bbox="340 1083 749 1161">jamii kubwa</td> <td data-bbox="749 1083 1153 1161">jamii ndogo</td> </tr> <tr> <td data-bbox="340 1161 749 1238">katiba nzuri</td> <td data-bbox="749 1161 1153 1238">katiba potovu</td> </tr> <tr> <td data-bbox="340 1238 749 1309">madhara makubwa</td> <td data-bbox="749 1238 1153 1309">madhara madogo</td> </tr> </tbody> </table>		Neno	Kinyume	mila nzuri	mila potovu	bahati nzuri	bahati mbaya	jamii kubwa	jamii ndogo	katiba nzuri	katiba potovu	madhara makubwa	madhara madogo
Neno	Kinyume													
mila nzuri	mila potovu													
bahati nzuri	bahati mbaya													
jamii kubwa	jamii ndogo													
katiba nzuri	katiba potovu													
madhara makubwa	madhara madogo													
	<table border="1"> <thead> <tr> <th data-bbox="422 1329 783 1402">Neno</th> <th data-bbox="783 1329 1144 1402">Kinyume</th> </tr> </thead> <tbody> <tr> <td data-bbox="422 1402 783 1476">Nzuri</td> <td data-bbox="783 1402 1144 1476">mbaya</td> </tr> <tr> <td data-bbox="422 1476 783 1549">Kubwa</td> <td data-bbox="783 1476 1144 1549">_____</td> </tr> <tr> <td data-bbox="422 1549 783 1622">Makubwa</td> <td data-bbox="783 1549 1144 1622">_____</td> </tr> <tr> <td data-bbox="422 1622 783 1696">Refu</td> <td data-bbox="783 1622 1144 1696">_____</td> </tr> <tr> <td data-bbox="422 1696 783 1769">Mrefu</td> <td data-bbox="783 1696 1144 1769">_____</td> </tr> </tbody> </table>		Neno	Kinyume	Nzuri	mbaya	Kubwa	_____	Makubwa	_____	Refu	_____	Mrefu	_____
Neno	Kinyume													
Nzuri	mbaya													
Kubwa	_____													
Makubwa	_____													
Refu	_____													
Mrefu	_____													



Mila na Tamaduni

Kila jamii kote duniani ina mila au utamaduni au desturi yao. Kuna mila nzuri na mila potovu. Mila nzuri hujenga na kufaidi jamii na watu binafsi. Mila potovu huleta madhara kwa maisha na maendeleo ya jamii husika. Kati ya mila nzuri ni kama vile watoto kutii wazazi wao na kuwasaidia kazi za nyumbani. Mila potovu ni kama kutahiri wasichana, ndoa za mapema, tabia za kuiba ng'ombe na kushiriki vita vya kijamii. Kwa bahati nzuri, Katiba mpya ya Kenya inatoa kanuni kabambe za kulinda kila Mkenya dhidi ya dhuluma zozote haswa zile zinazotokana na mila potovu.



Siku ya 5

	<p>a li mu o ke a alimuokea du bu dubu ma pa cha mapacha hu si ka husika n zu ri nzuri m go njwa mgonjwa mi la mila po to vu potovu mbwe ha mbweha</p>												
	<table border="1" style="display: inline-table; margin-right: 20px;"> <tr> <td>ma</td> <td>si</td> <td>ri</td> <td>m</td> </tr> <tr> <td>ri</td> <td>go</td> <td>pa</td> <td>ka</td> </tr> <tr> <td>hu</td> <td>nzu</td> <td>njwa</td> <td>cha</td> </tr> </table> <p>siri</p>	ma	si	ri	m	ri	go	pa	ka	hu	nzu	njwa	cha
ma	si	ri	m										
ri	go	pa	ka										
hu	nzu	njwa	cha										



Mkate Mtu



Somo ya 1

	<p>ma va zi ka nga ve li ka nzu bu i bu i ri nda shu ka s pe she li</p>	<p>mavazi kanga veli kanzu buibui rinda shuka spesheli</p>
	<p>hu tofautiana hu funika hu tumiwa hu valiwa hu patikana</p>	<p>hutofautiana hufunika hutumiwa huvaliwa hupatikana</p>


Somo ya 2

	<p>hutofautiana hufunikwa hupatikana</p>	<p>huvaliwa hutumiwa hujifunga</p>												
	<table border="1"> <thead> <tr> <th data-bbox="450 1358 761 1425">Mwanamke</th> <th data-bbox="761 1358 1093 1425">Mwanamme</th> </tr> </thead> <tbody> <tr> <td data-bbox="450 1425 761 1493">Rinda</td> <td data-bbox="761 1425 1093 1493"></td> </tr> <tr> <td data-bbox="450 1493 761 1561"></td> <td data-bbox="761 1493 1093 1561"></td> </tr> <tr> <td data-bbox="450 1561 761 1628"></td> <td data-bbox="761 1561 1093 1628"></td> </tr> <tr> <td data-bbox="450 1628 761 1696"></td> <td data-bbox="761 1628 1093 1696"></td> </tr> <tr> <td data-bbox="450 1696 761 1763"></td> <td data-bbox="761 1696 1093 1763"></td> </tr> </tbody> </table>		Mwanamke	Mwanamme	Rinda									
Mwanamke	Mwanamme													
Rinda														




Mavazi

Kuna mavazi mbalimbali ambayo huvaliwa na wanadamu. Mavazi haya hutofautiana kwa misingi ya utamaduni, dini, sherehe, kazi na hata hali ya anga.



Kwa mfano, kanzu huvaliwa na wanaume wa dini ya kiislamu. Nao wanawake waislamu huvalia mabuibui ambayo hufunika miili yao bila kuwabana. Watawa wa kike wakatoliki huvaa veli na marinda marefu. Kanga na shuka hutumiwa kama mavazi ya kitamaduni. Jina lingine la kanga ni leso na hupatikana kwa rangi mbalimbali. Leso huwa na ujumbe spesheli.



Siku ya 3

	i ba da ki le mba ko ti	ibada kilemba koti	ka nzu shu ka	kanzu shuka
	i li po wadia a li valia li li lo chakaa a li mu uliza	ilipowadia alivalia lililochakaa alimuuliza		
	<p style="text-align: center;">Kazi ya ziada:</p> Kanzu nyeupe Kanzu nyeusi Viatu vyeupe Viatu _____ Shuka nyekundu Shuka _____ Koti _____ Koti jeusi			

Siku ya 4


	wakati uliopita	wakati uliopo	wakati ujao		
	ilichakaa	inachakaa	itachakaa		
	alimuuliza	anamuuliza	atamuuliza		
	aliugua	anaugua	ataugua		
	aliaga	anaaga	ataaga		
	alivalia	anavalia	atavalia		
	<table style="width: 100%; border: none;"> <tr> <td style="width: 50%; border: none; vertical-align: top;"> Wakati uliopo anaaga _____ anavaa _____ anamuuliza _____ anashika </td> <td style="width: 50%; border: none; vertical-align: top;"> Wakati ujao ataaga ataugua _____ atacheza _____ atakutana _____ </td> </tr> </table>			Wakati uliopo anaaga _____ anavaa _____ anamuuliza _____ anashika	Wakati ujao ataaga ataugua _____ atacheza _____ atakutana _____
Wakati uliopo anaaga _____ anavaa _____ anamuuliza _____ anashika	Wakati ujao ataaga ataugua _____ atacheza _____ atakutana _____				



Siku ya Ibada

Siku ya Jumapili ilipofika Mzee Okelo alivalia kanzu yake nyeupe pepepe. Alijifunga kilemba chake kichwani na kuvalia viatu vyeusi. Alianza safari kuelekea kanisani. Njiani, alikutana na rafiki yake mzee Sakuda. Mzee Sakuda alikuwa amejifunga shuka nyekundu kiunoni na kotijeusi lililochakaa. “Mbona huendi kanisani leo?” Okelo alimuuliza rafiki yake. “Leo siendi kanisani. Naelekea kumwona shangazi yangu ambaye ameugua kwa muda mrefu.” Basi waliagana na mzee Okelo akashika njia moja kwa moja hadi kanisani.

Siku ya 5

	su ru a li	suruali
	ka p tu ra	kaptura
	b la u si	blausi
	fu la na	fulana



Mama afua nguo






Mama anafua nguo na kuzianika kwenye kamba. Maria anamtazama huku akitambua kila nguo inayoanikwa. Maria anasema, “Hii ni sare yangu ya kwenda shule.” Mama anaanika nguo zingine kwenye kamba. Maria

anasema, “Hii ni suruali ya kaka, Musa. Ijumaa, yeye alivaa suruali nyeusi na shati hii nyeupe tukaenda shuleni. Naye mama alivaa buibui na baba akavaa kanzu. Mama anatabasamu huku akiendelea kuanika nguo. Maria anaendelea kusema, “Shati hii ya mikono mirefu na kaptura ni za baba. Yeye huzivaa iwapo tunaenda matembezi. Nacho kilemba hiki ni cha mama na kanga pia.” Mama anamalizia kwa kuanika blausi na fulana mbili ndogo. Maria anampigia makofi na kusema, “Asante mama kwa kutufulia nguo. Tutang’ara kwelikweli.”

Siku ya 1

	<p>a li pa za wa li o sa li a ku mi</p>	<p>alipaza waliosalia kumi</p>
	<p>a li wa peleka wa li o salia ku wa rudishia wa na kijiji</p>	<p>aliwapeleka waliosalia kuwarudishia wanakijiji</p>

Siku ya 2

	<p>ki sha ma shu jaa vi ji to wa vu vi</p>	<p>kisha mashujaa vijito wavuvi</p>								
	<table border="1" style="margin-left: auto; margin-right: auto;"> <thead> <tr> <th data-bbox="481 1149 751 1226">Karibu</th> <th data-bbox="751 1149 1049 1226">Mbali</th> </tr> </thead> <tbody> <tr> <td data-bbox="481 1226 751 1296">msitu huu</td> <td data-bbox="751 1226 1049 1296">msitu ule</td> </tr> <tr> <td data-bbox="481 1296 751 1367">mkuki huu</td> <td data-bbox="751 1296 1049 1367">mkuki ule</td> </tr> <tr> <td data-bbox="481 1367 751 1439">mti huu</td> <td data-bbox="751 1367 1049 1439">mti ule</td> </tr> </tbody> </table>		Karibu	Mbali	msitu huu	msitu ule	mkuki huu	mkuki ule	mti huu	mti ule
Karibu	Mbali									
msitu huu	msitu ule									
mkuki huu	mkuki ule									
mti huu	mti ule									
	<p>mzee huyu mbuzi huyu pacha huyu ndege huyu</p>	<p>mzee huyo mbuzi huyo _____ _____</p>								





Mzee Ojwang'



Mzee Ojwang' alikuwa na mbuzi kumi. Aliwapeleka malishoni karibu na msitu mkubwa. Walipokuwa wakila nyasi, fisi akaja na kumla mmoja. Mzee Ojwang' alipaza sauti na kuita, "Wooiii. Nisaidie. Fisi! Mbuzi wangu! Wooooiii. Fisi! Mbuzi wangu!"


Wana kijiji wakaja haraka. Wengine walifukuza fisi huku wengine wakipiga simu kwa idara ya kulinda wanyama pori. Maafisa wa idara ya kulinda wanyama pori punde walifika lakini fisi tayari alikuwa amerudi kwenye msitu mkubwa. Wanakijiji walimsaidia Mzee Ojwang' kuwarudisha nyumbani mbuzi waliosalia. Keshoye, Mzee Ojwang' alijawa na furaha alipopata mbuzi wake wawili wamezaa mapacha.

Siku ya 3

	<p>a la ma he sa bu ku o nge za ku to a ku ga wa nya ku zi di sha ku ju m li sha ku sa wa zi sha</p>	<p>alama hesabu kuongeza ku to a kugawanya kuzidisha kujumlisha kusawazisha</p>
	<p>u ki vi jua ku vi elewa hu tu eleza</p>	<p>ukivijua kuvielewa hutueleza</p>

Siku ya 4

	<p>hudhani hugawanya hutoa</p>	<p>huongeza huzidisha hujumlisha</p>
	<p style="text-align: center;">Alama</p> <p>1. (+) _____ 2. _____ 3. (\div) _____ 4. _____ 5. (=) _____</p>	<p style="text-align: center;">Jina</p> <p>_____</p> <p>kutoa</p> <p>_____</p> <p>kuzidisha</p> <p>_____</p>



Alama za hesabu

Wanafunzi wengi hudhani kuwa somo la hesabu ni gumu sana. Ukweli ni kwamba somo hili sio gumu kama wanavyodhani. Kuna vitu kadhaa ambavyo ukivijua na kuvielewa basi hesabu huwa rahisi sana. La kwanza ni kujua alama za hesabu kama vile: Alama ya kuongeza (+), alama ya kutoa (-), alama ya kugawanya (\div), alama ya kuzidisha (\times) na alama ya kujumlisha (=). Alama hizi hukuelekeza kuhusu jinsi ya kutatua matatizo mbalimbali yanayohusisha hesabu. Kwa kijumla, somo hili hukupa ujuzi wa kuweza kufanya au kurahisisha kazi mbalimbali. Kwa hivyo tunaposoma hesabu sio tu kwa kufaulu katika mitihani yetu bali kwa ajili ya manufaa ya maisha ya baadaye. Ukitaka kufaulu maini lazima upende na kufanya bidii kwa somo hili la hesabu.

Siku ya 5



ma fu mbo	mafumbo
pa cha	pacha
nja ma	njama
ku nu ng'u ni ka	kunung'unika
wa wi nda ji	wawindaji

Mafumbo






Mimi ni muhimu.
Kila mtu
ananihitaji.
Ninamaliza kiu.
Ninatumika kwa
usafi. Mimi ni
nani?
Mimi ni mkubwa.
Ninaishi angani.
Natoa mwanga
duniani kote.

Nikilala giza huingia. Mimi ni nani?



Mimi ni rafiki wa kila kiumbe. Ninasafisha hewa. Nazaa matunda. Nawapatia binadamu kivuli. Mimi ni nani?


Mimi huishi msituni. Nina miguu minne. Mimi hula nyama. Wengine huniita mfalme. Mimi ni nani?

Siku ya 1

	ta ra ki mu i da di a ru ba i ni si ti ni sa bi ni ti si ni	tarakimu ida di arubaini sitini sabini tisini												
	i na itwa i na yo pendwa	inaitwa inayopendwa												
	<table border="1" style="width: 100%; text-align: center;"> <thead> <tr> <th style="width: 50%;">Jina</th> <th style="width: 50%;">Tarakimu</th> </tr> </thead> <tbody> <tr> <td>Mia tano na hamsini</td> <td>550</td> </tr> <tr> <td>Mia mbili na ishirini</td> <td>_____</td> </tr> <tr> <td>_____</td> <td>500</td> </tr> <tr> <td>Themanini</td> <td>_____</td> </tr> <tr> <td>_____</td> <td>60</td> </tr> </tbody> </table>		Jina	Tarakimu	Mia tano na hamsini	550	Mia mbili na ishirini	_____	_____	500	Themanini	_____	_____	60
Jina	Tarakimu													
Mia tano na hamsini	550													
Mia mbili na ishirini	_____													
_____	500													
Themanini	_____													
_____	60													

Siku ya 2




	1. Jumla la wanafunzi wa shule yetu ni mia mbili. 2. Idadi ya wanafunzi wa darasa la pili ni hamsini.			
	Tarakimu	Majina	Tarakimu	Majina
	100	Mia moja	300	
	200			
	220			





Tarakimu

Shule ya msingi ya Pomoni ina wanafunzi wengi. Jumla ya wanafunzi wa darasa la kwanza ni mia mbili. Idadi ya wasichana wa darasa la kwanza ni mia moja na wawili na ya wavulana ni tisini na wanane. Jumla ya wanafunzi wa darasa la pili ni mia nne na ishirini. Idadi ya wasichana wa darasa la pili ni mia tatu na ya wavulana ni mia moja ishirini. Jumla ya wanafunzi wa darasa la tatu ni mia tatu hamsini na saba. Idadi ya wasichana wa darasa la tatu ni mia mbili na ishirini na ya wavulana ni mia moja thelathini na saba. Jumla ya wanafunzi wa shule ya Pomoni ni mia tisa sabini na saba. Shule iliyo karibu na Pomoni inaitwa Ziwani. Shule ya msingi ya Ziwani ina wanafunzi mia tano peke yake. Wasichana ni mia mbili arubaini na wavulana ni mia mbili sitini. Shule inayopendwa sana ni Pomoni.

Siku ya 3

	ta re he tarehe na ne nane
	a li mu uliza alimuuliza a li agiza aliagiza a li m kabidhi alimkabidhi pa li ondokea paliondokea
	Tunga sentensi kutumia maneno haya: Dukani gazeti tarehe nyumbani

Siku ya 4

	Wakati Uliopita	Wakati Uliopo	Wakati Ujao	
	alimwita	anamwita	atamwita	
	aliuliza	anauliza	atauliza	
	alicheka	anacheka	atacheka	
	alichukua	anachukua	atachukua	
	aliitikia	anaitikia	ataitikia	
	alimkabidhi	anamkabidhi	atamkabidhi	
	Umoja		Wingi	
	Gazeti moja	1	Magazeti mawili	2
	Duka moja	1	Maduka mawili	2
	Gurudumu moja	1	Magurudumu mawili	2
			Magazeti _____	4
			Maduka _____	4
			Magurudumu _____	4

Gazeti la Baba

Paliondokea kijana mmoja aliyeitwa Romeo. Siku moja baba yake alimwita na kusema, “Romeo, nenda dukani uniletee gazeti la leo tarehe nane.” Romeo alichukua shilingi mia moja na kuelekea dukani. Alipofika kule alimuuliza mwenye duka, “Una gazeti la leo la tarehe nane?” Mwenye duka alijibu, “Sina.” Romeo aliuliza tena, “Je, unalo la tarehe nne?” Mwenye duka aliitikia kuwa alikuwa nalo.

Romeo aliagiza magazeti mawili ya tarehe nne na kuelekea nyumbani. Alipofika nyumbani, alimkabidhi babake yale magazeti mawili. Baba alipoona tarehe ni tofauti aliuliza, “Nani alikutuma magazeti mawili ya tarehe nne?” Romeo alisema, “Baba,



nilikosa gazeti la leo la tarehe nane. Lakini nilikumbuka kuwa nne mara mbili ni nane. Hivyo basi niliagiza mawili ya tarehe nne ili tupate tarehe nane.” Badala ya kukasirika baba alicheka na kusema, “Mwanangu, haiwi hivyo kwa gazeti. Ukiwa mkubwa, utaelewa.

Siku ya 5





mi a	mia
mbi li	mbili
wa wi li	wawili
n ne	nne
ku mi	kumi
e l fu	elfu
mi li o ni	milioni


Mzee Kabila




Siku ya 1

	<p>nye u pe nye u si ki ja ni ki bi chi nye ku ndu</p>	<p>nyeupe nyeusi kijani kibichi nyekundu</p>
	<p>i me ni lea ni ta i tetea tu li yo pigania wa ka hitimu</p>	<p>imenilea nitaitetea tuliyo pigania wakahitimu</p>

Siku ya 2

	<p>Wakati Uliopita</p>	<p>Wakati Uliopo</p>	<p>Wakati Ujao</p>
	alinilea	ananilea	atanilea
	alinisinya	ananisinya	atanisinya
	ilipepea	inapepea	itapepea
	ilimwagika	inamwagika	itamwagika
	alipenda	anapenda	atapenda
	ilibidi	inabidi	itabidi



Rangi za Bendera Yetu

Nchi yangu imenilea, Taifa langu la Kenya,
Nchi yangu taitetea, wabaya wamenisinya,
Bendera ikipepea, Wakenya twajivunia.



Rangi nne za bendera, ni muhimu nakwambia,
Nyeusi ya mwanadamu, uhuru kapigania,
Bendera ikipepea, Wakenya twajivunia.

Nyekundu ni ya damu, ilomwagika vitani,
Mashujaa wakahitimu, ukombozi usokifani,
Bendera ikipepea, Wakenya twajivunia.

Ya kijani rangi ya nchi, tulipigania hakika,
Tuipende daima nchi, vyovyote bila dhihaka,
Bendera ikipepea, Wakenya twajivunia,

Rangi nyeupe ya amani, kwa nini tusipendane?
Kumpenda wako jirani, hakuna hata jingine,
Bendera ikipepea, Wakenya twajivunia.

Siku ya 3

	be nde ra ma ri da di ki pe ke e	bendera maridadi kipekee
	i na wakilisha wa li o pigania u ki i tazama i li yo mwagika	inawakilisha waliopigania ukiitazama iliyomwagika

Siku ya 4



	<table border="1"> <thead> <tr> <th data-bbox="294 821 624 898">Wakati Uliopita</th> <th data-bbox="624 821 926 898">Wakati Uliopo</th> <th data-bbox="926 821 1207 898">Wakati Ujao</th> </tr> </thead> <tbody> <tr> <td data-bbox="294 898 624 966">iliwakilisha</td> <td data-bbox="624 898 926 966">inawakilisha</td> <td data-bbox="926 898 1207 966">itawakilisha</td> </tr> <tr> <td data-bbox="294 966 624 1033">walipigania</td> <td data-bbox="624 966 926 1033">wanapigania</td> <td data-bbox="926 966 1207 1033">watapigania</td> </tr> <tr> <td data-bbox="294 1033 624 1101">ilimwagika</td> <td data-bbox="624 1033 926 1101">inamwagika</td> <td data-bbox="926 1033 1207 1101">itamwagika</td> </tr> <tr> <td data-bbox="294 1101 624 1168">kilistawisha</td> <td data-bbox="624 1101 926 1168">kinastawisha</td> <td data-bbox="926 1101 1207 1168">kitastawisha</td> </tr> <tr> <td data-bbox="294 1168 624 1236">alimaanisha</td> <td data-bbox="624 1168 926 1236">anamaanisha</td> <td data-bbox="926 1168 1207 1236">atamaanisha</td> </tr> <tr> <td data-bbox="294 1236 624 1304">alikasirika</td> <td data-bbox="624 1236 926 1304">anakasirika</td> <td data-bbox="926 1236 1207 1304">atakasirika</td> </tr> </tbody> </table>			Wakati Uliopita	Wakati Uliopo	Wakati Ujao	iliwakilisha	inawakilisha	itawakilisha	walipigania	wanapigania	watapigania	ilimwagika	inamwagika	itamwagika	kilistawisha	kinastawisha	kitastawisha	alimaanisha	anamaanisha	atamaanisha	alikasirika	anakasirika	atakasirika
Wakati Uliopita	Wakati Uliopo	Wakati Ujao																						
iliwakilisha	inawakilisha	itawakilisha																						
walipigania	wanapigania	watapigania																						
ilimwagika	inamwagika	itamwagika																						
kilistawisha	kinastawisha	kitastawisha																						
alimaanisha	anamaanisha	atamaanisha																						
alikasirika	anakasirika	atakasirika																						
	<table border="1"> <thead> <tr> <th data-bbox="294 1362 761 1439">Wakati uliopo</th> <th data-bbox="761 1362 1207 1439">Wakati uliopita</th> </tr> </thead> <tbody> <tr> <td data-bbox="294 1439 761 1506">inawakilisha</td> <td data-bbox="761 1439 1207 1506">itawakilisha</td> </tr> <tr> <td data-bbox="294 1506 761 1574">anamaanisha</td> <td data-bbox="761 1506 1207 1574">_____</td> </tr> <tr> <td data-bbox="294 1574 761 1642">_____</td> <td data-bbox="761 1574 1207 1642">itamwagika</td> </tr> <tr> <td data-bbox="294 1642 761 1709">alimwaga</td> <td data-bbox="761 1642 1207 1709">_____</td> </tr> <tr> <td data-bbox="294 1709 761 1777">_____</td> <td data-bbox="761 1709 1207 1777">atafurahi</td> </tr> </tbody> </table>		Wakati uliopo	Wakati uliopita	inawakilisha	itawakilisha	anamaanisha	_____	_____	itamwagika	alimwaga	_____	_____	atafurahi										
Wakati uliopo	Wakati uliopita																							
inawakilisha	itawakilisha																							
anamaanisha	_____																							
_____	itamwagika																							
alimwaga	_____																							
_____	atafurahi																							

Bendera yetu

Kila taifa ulimwenguni lina bendera yake ya kipekee. Taifa letu la Kenya lina bendera iliyo na rangi nne. Kila rangi ina maana yake. Rangi ya kwanza ni nyeusi. Rangi nyeusi inawakilisha rangi ya Wakenya. Wakenya, kama watu wengine barani Afrika, ni watu weusi. Sio weupe kama wazungu. Rangi ya pili ni nyekundu. Rangi hii nyekundu inawakilisha ushujaa wa wazalendo waliopigania uhuru wetu. Wakati mwingine husemwa kuwa inawakilisha damu iliyomwagika tukiupigania uhuru wa Kenya. Rangi ya tatu ni kijani kibichi. Rangi hii inawakilisha kilimo cha nchi yetu. Kilimo hustawisha uchumi wa nchi yetu. Rangi ya nne ya bendera yetu ni rangi nyeupe. Rangi hii inawakilisha amani ya nchi yetu. Ukiitazama bendera ya Kenya ikipepea, ni maridadi kabisa



Siku ya 5

	<p>m li nzi u s ta wi ngu vu wa ji bu i s ta hi li shu k ra ni</p>	<p>m linzi ustawi nguvu wajibu istahili shukrani</p>
	<p>ustawi uhuru wajibu umoja</p>	<p>wetu _____ _____ _____</p>

Wimbo wa Taifa

Ee Mungu nguvu yetu,
Ilete baraka kwetu,
Haki iwe ngao na mlinzi,
Natukae na undugu,
Amani na uhuru,
Raha tupate na ustawi.



Amkeni ndugu zetu,
Tufanye sote bidii,
Nasi tujitoe kwa nguvu,
Nchi yetu ya Kenya,
Tunayoipenda,
Tuwe tayari kuilinda.

Natujenge taifa letu,
Ee ndio wajibu wetu,
Kenya istahili heshima,
Tuungane mikono,
Pamoja kazini,
Kila siku tuwe na shukrani.


Siku ya 1

	ie bwa gha nga	-ea mju cha ngu	nywa mb mre ndi	ua cha mvu	uu che nchi
	wakiogelea rangi nyumbani zilivyo	kitambo kubwa waling'amua kwenye	alimuuliza mrefu mvua wamejificha	mjukuu gharika kioo mbingu	
	Kazi ya ziada:				
	Aliwaza sana _____		Aliona watu _____		
	Aliwaletea zawadi _____		Alitoka nje _____		

Siku ya 2

	mwo ao io	mgo vya ia	ie au ngwa	ea aa bwa	ii ai												
	<table border="1" style="width: 100%; border-collapse: collapse;"> <thead> <tr> <th style="width: 50%; text-align: center;">Umoja</th> <th style="width: 50%; text-align: center;">Wingi</th> </tr> </thead> <tbody> <tr> <td>kipande kikubwa</td> <td>vipande vikubwa</td> </tr> <tr> <td>kicheko kikubwa</td> <td>_____</td> </tr> <tr> <td>_____</td> <td>viatu vikubwa</td> </tr> <tr> <td>kitu kikubwa</td> <td>_____</td> </tr> <tr> <td>kikapu kikubwa</td> <td>_____</td> </tr> </tbody> </table>					Umoja	Wingi	kipande kikubwa	vipande vikubwa	kicheko kikubwa	_____	_____	viatu vikubwa	kitu kikubwa	_____	kikapu kikubwa	_____
Umoja	Wingi																
kipande kikubwa	vipande vikubwa																
kicheko kikubwa	_____																
_____	viatu vikubwa																
kitu kikubwa	_____																
kikapu kikubwa	_____																

Kwa nini Mbingu ni Samawati



Siku moja Rehema alikuwa baharini na bibi wakiogelea. Rehema alimuuliza bibi, “Mbona maji ya bahari ni yana rangi ya samawati na yale yaliyoko nyumbani hayana rangi hiyo?” Bibi aliwaza kwa kitambo kidogo. Alipofungua


kinywa chake tena alisema: Mjukuu wangu, hebu nikusimulie hadithi. Sikiza kwa makini.

Hapo zamani za kale kulitokea mvua kubwa sana Mvua hiyo ilinyesha kwa muda mrefu na kuleta mafuriko. Mafuriko hayo yalisababisha gharika. Watu wengi waliangamia. Walionusurika ni wale waliojificha kwenye safina maalum. Maji yalitapakaa kote hadi yakapita mawingu na kugusa mbingu. Siku hizo, maji yalikuwa na rangi ya samawati . Pindi tu yalipogusa mbingu, mbingu hizo zilipata rangi hiyo ya samawati. Wakati huo huo, maji hayo yalipoteza rangi yake. Yaliporudi chini, hayakuwa na rangi ya samawati tena. Nchi ilipokauka, watu waliokuwa wamejificha kwenye safina walitoka nje. Walipoangalia juu angani, waliona rangi ya mbingu zimebadilika na kuwa samawati. Walipochota maji nyumbani, waliona hayana rangi yoyote. Baadaye watu hawa waling’amua kuwa maji ya bahari au ziwa au hata bwawa huwa kama kioo kinachoonyesha mbingu zilivyo. Ndio maana maji haya ya bahari yanaonekana yana rangi ya samawati ilhali ukiyachota hayana.

Siku ya 3

	m k u mku ny w as nywa m sh a msha gh a gha																			
	mkulima nguruwe	mweusi mayai	ng'ombe soseji	nguruwe maziwa																
	<table border="1"> <thead> <tr> <th>Nomino</th> <th>rangi nyeusi</th> <th>rangi nyekundu</th> <th>rangi nyeupe</th> </tr> </thead> <tbody> <tr> <td>Ng'ombe</td> <td>mweusi</td> <td>mwekundu</td> <td>mweupe</td> </tr> <tr> <td>Kuku</td> <td></td> <td></td> <td></td> </tr> <tr> <td>Nguruwe</td> <td></td> <td></td> <td></td> </tr> </tbody> </table>				Nomino	rangi nyeusi	rangi nyekundu	rangi nyeupe	Ng'ombe	mweusi	mwekundu	mweupe	Kuku				Nguruwe			
Nomino	rangi nyeusi	rangi nyekundu	rangi nyeupe																	
Ng'ombe	mweusi	mwekundu	mweupe																	
Kuku																				
Nguruwe																				

Siku ya 4



	<p>Kazi ya Ziada: Tumia mfano huu kujaza pengo zifuatazo ukitumia angu, ako na ake.</p>		
	-angu	-ako	-ake
	Sare yan gu	Sare ya ko	Sare ya ke
	Suruali yan gu		
	Kanzu yan gu		



Mama afua nguo

Mama anafua nguo na kuzianika kwenye kamba. Maria anamtazama huku akitambua kila nguo inayoanikwa. Maria anasema, “Hii ni sare yangu ya kwenda shule.” Mama anaanika nguo zingine kwenye kamba. Maria anasema, “Hii ni suruali ya kaka, Musa. Ijumaa, yeye alivaa suruali nyeusi na shati hii nyeupe tukaenda shuleni. Naye mama alivaa buibui na baba akavaa kanzu wakaelekea msikitini kuswali.” Mama anatabasamu huku akiendelea kuanika nguo. Maria anaendelea kusema, “Shati hii ya mikono mirefu na kaptura ni za baba. Yeye huzivaa iwapo tunaenda matembezi. Nacho hiki kilemba na kanga hii ni vya mama.” Mama anamalizia kwa kuanika blauzi na fulana mbili ndogo. Maria anampigia makofi na kusema, “Asante mama kwa kutufulia nguo. Tutang’ara kwelikweli.”

Siku ya 5

	<p>gha ri ka gharika ki pa nde kipande mku li ma mkulima m vu a mvua vi a tu viatu ma ya i mayai</p>																
	<table border="1" data-bbox="391 608 864 975"> <tr> <td>gh</td> <td>ya</td> <td>ki</td> <td>a</td> </tr> <tr> <td>vi</td> <td>mku</td> <td>ri</td> <td>nde</td> </tr> <tr> <td>li</td> <td>pa</td> <td>m</td> <td>i</td> </tr> <tr> <td>ma</td> <td>ku</td> <td>tu</td> <td>ka</td> </tr> </table> <p>yai</p>	gh	ya	ki	a	vi	mku	ri	nde	li	pa	m	i	ma	ku	tu	ka
gh	ya	ki	a														
vi	mku	ri	nde														
li	pa	m	i														
ma	ku	tu	ka														

Fisi na sungura

